JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI

**TUME YA MIPANGO**



# MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2025/26

**Novemba, 2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI**

**TUME YA MIPANGO**

# MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2025/26

**Novemba, 2024**

# Yaliyomo


ORODHA YA VIFUPISHO i

YALIYOMO ii

**SURA YA KWANZA**

UTANGULIZI 1

1.1 Usuli 1

1.2 Mawanda na Mafanikio ya Utekelezaji wa Vipaumbele 2

1.3 Malengo ya Mapendekezo ya Mpango 4

1.4 Ugharamiaji wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2025/26 4

1.5 Maandalizi ya Mpango 5

1.6 Mpangilio wa Kitabu 5

**SURA YA PILI**

HALI YA UCHUMI 7

2.1 Utangulizi 7

2.2 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Dunia na Kikanda 7

2.2.1 Ukuaji wa Uchumi wa Dunia 7

2.2.2 Ukuaji wa Uchumi wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara 8

2.2.3 Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika 9

2.2.4 Mfumuko wa Bei wa Dunia 11

2.2.5 Mfumuko wa Bei wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika 11

2.2.6 Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki 11

2.3 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa 12

2.3.1 Ukuaji wa Uchumi wa Taifa 12

2.3.2 Mfumuko wa Bei Nchini 15

2.3.3 Sekta ya Nje 15

2.3.4 Sekta ya Fedha 16

2.3.5 Deni la Serikali 17

2.3.6 Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu 17

*2.3.6.1 Hali ya Umaskini 17*

*2.3.6.2 Maendeleo ya Watu 19*

*2.3.6.3 Idadi ya Watu 20*

2.4 Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025/26 26

2.4.1 Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi Jumla 21
2.4.2 Misingi (Assumptions) ya Mpango kwa Mwaka 2025/26 21

**SURA YA TATU**
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO 23
3.1 Utangulizi 23
3.2 Utekelezaji wa Vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano katika Mwaka 2023/24 na Utekelezaji katika Kipindi cha Robo ya Kwanza Mwaka 2024/25 23
3.2.1 Miradi ya Kielelezo 23
*3.2.1.1 Miundombinu ya Usafirishaji* 24
*3.2.1.2 Kuboresha Shirika la Ndege* 25
3.2.1.3 *Miundombinu ya Nishati* 25
3.2.1.4 *Miradi ya Kuongeza Uzalishaji Viwandani* 26
3.2.2 Programu na Miradi ya Kimkakati ya Kisekta 27
*3.2.2.1 Sekta ya Ujenzi* 27
*3.2.2.2 Sekta ya Uchukuzi* 28
*3.2.2.3 Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari* 30
*3.2.2.4 Sekta ya Nishati* 31
*3.2.2.5 Sekta ya Kilimo* 33
*3.2.2.6 Sekta ya Mifugo* 35
*3.2.2.7 Sekta ya Uvuvi* 36
*3.2.2.8 Sekta ya Uzalishaji Bidhaa Viwandani* 38
*3.2.2.9 Sekta ya Madini* 39
*3.2.2.10 Sekta ya Mazingira na Maliasili Asilia* 40
*3.2.2.11 Sekta ya Utalii* 41
*3.2.2.12 Sekta ya Sanaa, Michezo na Ubunifu* 43
*3.2.2.13 Sekta ya Kukuza Uwekezaji na Biashara* 45
*3.2.2.14 Sekta ya Diplomasia ya Uchumi* 47
*3.2.2.15 Sekta ya Elimu na Maendeleo ya Ujuzi* 48
*3.2.2.16 Sekta ya Afya* 50
*3.2.2.17 Sekta ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira* 51
*3.2.2.18 Sekta ya Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi* 53
*3.2.2.19 Sekta ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii* 54
*3.2.2.20 Kuendeleza Ujuzi* 55


**SURA YA NNE**
VIPAUMBELE NA MALENGO KWA MWAKA 2025/26 59
4.1 Utangulizi 59
4.2 Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi 60
4.3 Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma 61
4.4 Kukuza Uwekezaji na Biashara 62
4.5 Kuchochea Maendeleo ya Watu 62
4.6 Kuendeleza Ujuzi 63

**SURA YA TANO**
UFUATILIAJI, TATHMINI NA VIHATARISHI 65
5.1 Utangulizi 65
5.2 Ufuatiliaji na Tathmini 66
5.2.1 Matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini 66
5.2.2 Muundo wa Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini 66
5.2.3 Mgawanyo wa Majukumu katika Ufuatiliaji na Tathimini 66
5.3 Vihatarishi na Mikakati ya Kukabiliana Navyo kwa Mwaka 2025/2026 67
5.3.1 Vihatarishi vya Ndani na Nje 67
5.3.2 Mikakati ya Kukabiliana na Vihatarishi 67

# Orodha ya Vifupisho

| | |
|---|---|
| **ADC** | Aquaculture Development Centres |
| **ATCL** | Air Tanzania Company Limited |
| **CBR** | Central Bank Rate |
| **CNG** | Compressed Natural Gas |
| **DRC** | Democratic Republic of Congo |
| **EAC** | East Africa Community |
| **EIA** | Environment Impact Assessment |
| **FYDP III** | Third Five Year Development Plan |
| **Ha** | Hectare |
| **IMF** | International Monetary Fund |
| **JNHPP** | Julius Nyerere Hydropower Plant |
| **KM** | Kilometer |
| **KWh** | Kilowatt Hour |
| **LNG** | Liquefied Natural Gas |
| **MW** | Megawatt |
| **NHIF** | National Health Insuarance Fund |
| **NPMIS** | National Project Management Information System |
| **NRW** | Non-revenue Water |
| **PIM-OM** | Public Investment Management Operational Manual |
| **PPP** | Public-Private Partnership |
| **PSSN** | Productive Social Safetynet |
| **SADC** | Southern African Development Community |
| **SDGs** | Sustainable Development Goals |
| **SGR** | Standard Gauge Railway |
| **TASAF** | Tanzania Social Action Fund |
| **TaSUBa** | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo |
| **TAZARA** | Tanzania - Zambia Railway Authority |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **U&T** | Ufuatiliaji na Tathmini |
| **USD** | United State Dollar |
| **UVIKO – 19** | Ugonjwa wa Virusi vya Korona - 2019 |
| **VVU** | Virusi Vya Ukimwi |

## SURA YA KWANZA






# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 ni wa tano (5) na wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 (FYDP III) ambayo ina dhima ya **Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu**. Maandalizi ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2025/26 yamezingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Muda Mrefu wa Maendeleo (2011/12 - 2025/26), Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020; Agenda ya Maendeleo ya Afrika 2063, Agenda 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu; na makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi. Aidha, Mapendekezo haya yamezingatia matokeo ya mapitio ya utekelezaji wa mipango ya taifa ya maendeleo ya kila mwaka ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Tathmini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, maendeleo na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kijamii duniani, mabadiliko ya tabianchi na mageuzi ya kidijitali yanayoendelea duniani.

Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya kila mwaka hutumika kama nyenzo muhimu ya kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Utekelezaji huo unahusisha uainishaji na utekelezaji wa afua, miradi na shughuli kila mwaka pamoja na kuimarisha ufuatiliaji na tathmini kwa kupima hatua zilizofikiwa ikilinganishwa na malengo yaliyowekwa ifikapo mwaka 2025/26. Aidha, utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya 2023/24 na 2024/25 ni mwendelezo wa utekelezaji wa Mipango iliyotangulia ambayo imechangia kuleta mafanikio katika sekta mbalimbali na maendeleo ya watu. Vile vile, uchambuzi wa msingi kuonesha hali ya ujumla ya mwenendo wa utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III) umebainishwa ili kuonesha picha ya utekelezaji kwa ujumla.

## 1.2 Mawanda na Mafanikio ya Utekelezaji wa Vipaumbele

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2025/26 yamejikita katika maeneo ya kipaumbele yafuatayo: kuchochea uchumi shirikishi na shindani; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza uwekezaji na biashara; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza ujuzi. Maeneo haya ya kipaumbele yamelenga kuhakikisha mwendelezo wa Mipango ya muda wa kati ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye hadhi ya uchumi wa kipato cha kati kwa kuchochea ukuaji wa kiuchumi na kuendeleza mageuzi ya viwanda. Hivyo, watekelezaji wa afua mbalimbali za maendeleo watahitajika kuelekeza rasilimali katika mwaka 2025/26 kwenye hatua muhimu (key interventions) za Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26.

Uainishaji wa maeneo mahsusi ya vipaumbele yamezingatia hatua za utekelezaji katika kufikia malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, mipango ya kisekta, taarifa za tafiti na Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022; na mabadiliko ya mwenendo wa kiuchumi na kijamii. Kulingana na matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, idadi ya watu imeongezeka kwa kiwango cha asilimia 3.2 kwa mwaka sawa na ongezeko la watu takribani milioni 1.7 kwa mwaka. Kasi hii ya ukuaji inaashiria uhitaji na umuhimu wa kuendelea kutoa kipaumbele katika sekta za huduma za jamii ikijumuisha sekta za afya, maji, elimu, uwezeshaji wa jamii hususan wanawake na vijana, pamoja na masuala ya udhibiti na usimamizi wa matumizi ya maliasili na utunzaji wa mazingira.

**3.2%**

*Kiwango cha aslimia cha ongezeko la watu kulingana na matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi*

Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Mwaka 2025/26 yanaandaliwa wakati utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ukielekea ukingoni. Serikali ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Dira 2025 na tathmini husika ilijikita katika nguzo kuu tano (5) ambazo ni: kuboresha hali ya maisha ya Watanzania; kuwepo kwa mazingira ya amani, utulivu na umoja; kujenga utawala bora na utawala wa sheria; kujenga uchumi imara unaoweza kuhimili ushindani; na kujenga jamii iliyoelimika na inayopenda kujifunza.



Tathmini imebainisha kuwa: kwa sasa nchi ina utoshelevu wa chakula kwa asilimia 124 ikilinganishwa na lengo la asilimia 140 ifikapo 2025; wastani wa pato kwa mtu limeongezeka kutoka dola za Marekani 399.5 mwaka 2000 hadi dola za Marekani 1,276.8 mwaka 2023. Ongezeko hii limeifanya Tanzania kuendelea kuwa katika kundi la nchi zenye hadhi ya kipato cha kati cha chini. Vilevile, umri wa kuishi umeongezeka kutoka wastani wa miaka 51 mwaka 2002 hadi wastani wa miaka 66 kwa mwaka 2022 na unakadiriwa kuwa. Kwa upande wa viashiria vya elimu, utolewaji wa elimu ya msingi kwa wote umeimarika kufikia asilimia 97 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 69 mwaka 1999 huku kiwango cha kumaliza shule kikiongezeka hadi asilimia 69 mwaka 2022 kutoka asilimia 51 mwaka 2000. Maeneo mengine ambayo Dira ya 2025 imefanikiwa ni pamoja na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 750 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2000 hadi vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022.

Kwa msingi huo, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 imedhihirisha kuwa maisha ya Watanzania yameimarika ikilinganishwa na zaidi ya miaka 23 iliyopita katika nyanja zote za elimu, afya, miundombinu, uchukuzi na hali ya maisha. Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 yataimarisha mafanikio haya ya Dira ya 2025 na kujenga msingi imara wa Dira Mpya ya Taifa ya Maendeleo 2050 inayoandaliwa.

Ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Serikali imeweka nguvu kubwa kwenye utekelezaji na ukamilishaji wa miradi ya Kielelezo ambayo inawezesha nchi kupata matokeo makubwa ya kiuchumi na kijamii. Mkazo zaidi uliwekwa katika ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR) ambayo imeanza kufanya kazi na kuitangaza nchi kimataifa, kupunguza muda wa kusafiri na hivyo kusaidia shughuli za kiuchumi.

Miradi mingine ya Kielelezo iliyotekelezwa ni ufufuaji wa Shirika la Ndege Tanzania ambapo jumla ya ndege 16 zimenunuliwa kati ya ndege 19 zilizopangwa kununuliwa ifikapo 2025/26 sawa na asilimia 84 ya kufikia lengo. Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115 ambao kwa sasa unachangia megawati 740 katika gridi ya taifa na kuimarisha upatikanaji wa umeme kunakowezesha utekelezaji wa shughuli za uzalishaji. Ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima (Uganda) hadi bandari ya Tanga eneo la Chongoleani; na uwekezaji wa kongane za viwanda kupitia maeneo maalumu ya uwekezaji. Ukamilishaji wa miradi hii utakuwa kichocheo kikubwa kwa sekta nyingine, uzalishaji wa ajira na kufungua maeneo yaliyokuwa nyuma kiuchumi na kijamii.

**$1,276.8**
**2023** *wastani wa pato kwa mtu limeongezeka*

**$399.5**
**2000** *wastani wa pato kwa mtu mwaka huo*

**miaka 66**
**2022** *wastani wa umri wa kuishi umeongezeka*

**miaka 51**
**2002** *wastani wa umri wa kuishi mwaka huo*

*kupungua kwa idadi ya vifo vya wajawazito kutoka vifo **7500** kwa mwaka hadi **104***

**16**
**2024**
*ndege zilizonunuliwa tayari*

**2,115**
**megawatts**
*Mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere*

## 1.3 Malengo ya Mapendekezo ya Mpango

Mapendekezo haya yanatoa msingi wa maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26. Mkazo utawekwa katika kuhimiza utekelezaji wa pamoja na kufungamanisha matokeo ya Kitaifa kwa ujumla hususan katika kufanikisha malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Malengo Mahsusi ya Mapendekezo ya Mpango ni:**

i. Kuendelea na uimarishaji wa uwekezaji katika sayansi, teknolojia, na uwezo wa ubunifu ili kuhakikisha nchi inatoka kwenye nafasi ya fursa linganifu hadi kuwa na fursa shindani;
ii. Kuendelea kuwekeza katika utafiti na matumizi ya matokeo ya tafiti kwa lengo la kufanya mageuzi katika sekta za uzalishaji;
iii. Kuendelea kuimarisha viashiria vya uchumi jumla ili kuwa na uchumi imara na stahimilivu;
iv. Kukamilisha miradi ya kielelezo na kimkakati yenye matokeo makubwa kiuchumi;
v. Kuimarisha ushirikiano na Sekta Binafsi kwa kuboresha mazingira ya biashara ili kuchochea uanzishwaji wa biashara pamoja na kuvutia uwekezaji nchini na hivyo kuongeza upatikanaji wa ajira;
vi. Kuendelea kuimarisha amani na utulivu wa kisiasa nchini pamoja na usalama wa Watanzania; na
vii. Kuhakikisha rasilimali za nchi ikiwemo maji, ardhi, nishati na madini zinatumika katika namna ya uendelevu na kuchochea ufikiwaji wa malengo yaliyoanishwa.

## 1.4 Ugharamiaji wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2025/26

Katika mwaka 2025/26, Serikali inatarajia kutumia kiasi cha shilingi bilioni 16,459.43 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za maendeleo. Ugharamiaji huo utatokana na vyanzo mbalimbali ikiwemo mapato ya ndani, misaada, mikopo ya ndani yenye masharti ya kibiashara na mikopo ya nje yenye masharti nafuu. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha ugharamiaji wa miradi kupitia njia bunifu za ugharamiaji kwa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji na kuendelea kuimarisha mifumo ya kisheria na kitaasisi ya ubia baina ya sekta binafsi na umma. Lengo ni kukuza ushirikiano na ushiriki wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo.

**bil. 16,459**
**2025/26**
*gharama za serikali kwa shughuli mbalimbali za maendeleo*


## 1.5 Maandalizi ya Mpango

Maandalizi ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 yamehusisha wadau mbalimbali kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma na Sekta Binafsi. Ushirikishwaji wa makundi tajwa ulifanyika kwa njia mbalimbali ikiwemo vikao vya majadiliano, uandishi na uhariri. Aidha, takwimu zilizoainishwa katika mapendekezo haya zimetokana na tafiti, taarifa za utekelezaji za sekta, machapisho mbalimbali ya kisayansi na kitaalamu ya ndani na nje ya nchi.

## 1.6 Mpangilio wa Kitabu

Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango kimegawanyika katika sura tano (5): **Sura ya Kwanza:** utangulizi ambao unajumuisha usuli, malengo ya mapendekezo na maandalizi; **Sura ya Pili:** inaelezea mapitio ya hali ya uchumi; **Sura ya Tatu:** inatoa uchambuzi wa msingi wa mwenendo wa utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III); **Sura ya Nne:** inaelezea vipaumbele kwa mwaka 2025/26; na **Sura ya Tano:** inaainisha ufuatiliaji, tathmini na vihatarishi

# SURA YA PILI





# HALI YA UCHUMI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea mwenendo wa viashiria vya uchumi kitaifa, kikanda, na kimataifa kwa mwaka 2023 pamoja na mwelekeo kwa mwaka 2024 na 2025. Uchambuzi wa viashiria vya uchumi na mwenendo wake ni muhimu katika kupanga maendeleo ya taifa kwa kuwa inawezesha kulinganisha mwenendo wa uchumi wa nchi na uchumi wa dunia kwa ajili ya kupendekeza sera sahihi. Aidha, uchambuzi wa viashiria vya uchumi jumla vilivyotokea na vinavyotokea unajenga msingi imara wa kuandaa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26. Viashiria vilivyofanyiwa mapitio ni pamoja na: pato la taifa; mfumuko wa bei; mwenendo wa sekta ya nje; sekta ya fedha; deni la Serikali; na viashiria vya maendeleo ya watu ikiwemo idadi ya watu na hali ya umaskini nchini.

## 2.2 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Dunia na Kikanda

### 2.2.1 Ukuaji wa Uchumi wa Dunia

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya mwezi Julai 2024, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia imeendelea kupungua hadi kufikia asilimia 3.3 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2022. Upungufu huo ulitokana na sababu mbalimbali ikiwemo kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi wa nchi zinazoibukia na zilizoendelea za Asia, kudorora kwa mnyororo wa ugavi, na madhara yatokanayo na migogoro na mivutano ya kisiasa

**3.3%**
**(2023)**
*ukuaji wa uchumi wa dunia umepungua*

**3.5%**
**(2022)**

katika maeneo mbalimbali pamoja na sera za kupunguza ukwasi hususan katika nchi ya Marekani na chumi za Ulaya ili kukabiliana na mfumuko wa bei. Kwa upande mwingine, uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.2 na 3.3 mwaka 2024 na 2025 mtawalia. Kasi hii ndogo ya ukuaji wa uchumi, hususan kwa nchi zilizoendelea, inaashiria matumizi ya sera za fedha zinazolenga kupunguza ukwasi katika uchumi na kupungua kwa misaada kwa nchi zinazoendelea.

### 2.2.2 Ukuaji wa Uchumi wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara

Ukuaji wa uchumi wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ulipungua hadi kufikia wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 4.0 mwaka 2022. Upungufu huu ulitokana na utekelezaji wa sera ya kupunguza ujazi wa fedha kwenye uchumi wa Marekani ili kukabiliana na mfumuko wa bei, hivyo kusababisha uhaba wa fedha za kigeni katika nchi zinazoendelea hususan dola ya Marekani, kushuka kwa thamani ya fedha dhidi ya dola ya Marekani, kuongezeka kwa gharama za mikopo katika masoko ya fedha ya kikanda na kimataifa na kupungua kwa mauzo ya bidhaa kutoka nchi za Afrika kufuatia kupungua kwa uhitaji kutoka nchi washirika wakuu wa kibiashara. Aidha, uchumi kwa nchi za Kusini mwa Afrika mwa Jangwa la Sahara ulipungua kutokana na athari za muda mrefu za janga la UVIKO - 19 pamoja na uwiano hasi wa bei za bidhaa zinazouzwa na kununuliwa nje ya bara la Afrika. Aidha, uchumi wa nchi hizi unatarajiwa kuongezeka na kufikia ukuaji wa asilimia 3.7 mwaka 2024 na kuendelea kukua na kufikia asilimia 4.1 mwaka 2025.


▼ **3.4%**
**(2023)**
*kiwango cha ukuaji wa uchumi wa nchi za kusini kimepungua*

▲ **4.0%**
**(2022)**

▲ **3.7%**
**(2024)**
*kiwango cha ukuaji wa uchumi wa nchi za kusini kinachotarajiwa*

▲▲ **4.1%**
**(2025)**
*kiwango cha ukuaji wa uchumi wa nchi za kusini kinachotarajiwa*

**Kielelezo Na. 1.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Dunia na Matarajio**





***Chanzo:*** *Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF - WEO), Julai 2024.*

## 2.2.3 Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika


Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Julai, 2024 kiwango cha ukuaji wa pato la taifa kwa nchi za ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ulikuwa kwa wastani wa asilimia 4.6 na asilimia 3.9 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.2 na asilimia 5.0 mwaka 2022 mtawalia. Kupungua kwa ukuaji kulitokana na kuongezeka kwa mfumuko wa bei, kuongezeka kwa gharama za ukopaji katika masoko ya fedha ya kimataifa, kupungua kwa misaada na mikopo nafuu, athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja mgogoro unaoendelea kati ya Urusi na Ukraine. Aidha, Kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa jumuiya hizo kinatarajiwa kufikia asilimia 5.4 kwa EAC na asilimia 3.7 kwa SADC katika mwaka 2024 kama inavyoonekana katika kielelezo Na.1.2 na 1.3.

**4.6%**
**3.9%**
**(2023)**
*kiwango cha ukuaji wa uchumi wa nchi za ukanda wa jumuiya ya Afrika mashariki kimepungua*

**4.2%**
**5.0%**
**(2022)**




*Chanzo:* *Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) toleo la Julai, 2024*




*Chanzo:* *Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) toleo la Julai, 2024*

### 2.2.4 Mfumuko wa Bei wa Dunia

Mwaka 2023, mfumuko wa bei wa dunia ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 6.7 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 8.7 mwaka 2022. Kupungua kwa kasi ya ongezeko la bei za bidhaa na huduma duniani kulitokana na kuimarika kwa bei ya bidhaa, hususan nishati. Matarajio ya mfumuko wa bei wa Dunia utaendelea kupungua na kufikia asilimia 5.9 mwaka 2024 na asilimia 4.4 mwaka 2025. Aidha, mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.3 mwaka 2022. Vile vile, mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 8.3 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 9.8 mwaka 2022.

**6.7%**
**(2023)**
*mfumuko wa bei wa dunia*

**8.7%**
**(2022)**

### 2.2.5 Mfumuko wa Bei wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Aprili, 2024 mfumuko wa bei kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 16.2 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 14.5 mwaka 2022. Ongezeko la mfumuko wa bei lilitokana na sababu mbalimbali zikiwemo kupungua kwa ugavi wa mazao ya chakula katika baadhi ya masoko ya kikanda, kuongezeka kwa wastani wa bei za mafuta na mbolea kwa baadhi ya nchi hizo, pamoja na kasi ya kushuka kwa thamani ya sarafu kuliko ilivyotarajiwa. Nchi zilizokuwa na mfumuko wa bei wa juu ni pamoja na Zimbabwe (asilimia 667.4), Sudani ya Kusini (asilimia 40.2), Ghana (asilimia 37.5), Malawi (asilimia 30.3) na Ethiopia (asilimia 30.2). Aidha, kwa mwaka 2024 mfumuko wa bei kwa nchi hizo unatarajiwa kuwa wa wastani wa asilimia 15.3. Kwa upande wa mfumuko wa bei kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ulikuwa wastani wa asilimia 50.3 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 21.4 mwaka 2022.

**16.2%**
**(2023)**
*mfumuko wa bei kwa nchi za kusini mwa jangwa la sahara umeongezeka*

**14.5%**
**(2022)**
*mfumuko wa bei kwa nchi za kusini mwa jangwa la sahara ulikuwa chini*


### 2.2.6 Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki

Mwaka 2023, mfumuko wa bei kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 16.9 ikilinganishwa na asilimia 8.3 mwaka 2022. Nchi zilizoongoza kuwa na mfumuko wa bei kwa kiwango kikubwa ni: Sudan Kusini (40.2) Burundi (asilimia 27.0) na DRC (asilimia 19.9). Ongezeko hilo lilitokana na kupungua kwa ugavi wa mazao ya chakula katika baadhi ya masoko ya kikanda, kuongezeka kwa wastani wa bei za mafuta na mbolea kwa baadhi ya nchi. Aidha, kwa wastani, viwango vya mfumuko wa bei kwa nchi ya Tanzania, Kenya na Uganda ndivyo pekee viliendelea kuwa ndani ya lengo la Jumuiya la mfumuko wa bei wa kiwango cha kati ya asilimia 3.0 hadi 7.0 kwa mwaka. Kielelezo Na.1.4 kinaonesha mfumuko wa bei katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Mwaka 2023.

**16.9%**
**(2023)**
*mfumuko wa bei kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umeongezeka*

**8.3%**
**(2022)**
*mfumuko wa bei kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa chini*

**Kielelezo Na. 1.4: Mfumuko wa Bei katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Mwaka 2022 - 2023 na Matarajio mwaka 2024**




***Chanzo:*** *Ofisi za Taifa za Takwimu za nchi husika*

## 2.3 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa

### 2.3.1 Ukuaji wa Uchumi wa Taifa

Mwaka 2023, Pato halisi la Taifa kwa bei za mwaka 2015 lilifikia shilingi billioni 148,399.76 kutoka shilingi billioni 141,247.19 mwaka 2022, sawa na ukuaji wa asilimia 5.1 ikilinganishwa na asimilia 4.7 mwaka 2022. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na shughuli za kilimo, ujenzi na uchimbaji madini. Ukuaji wa sekta ya kilimo umechangiwa zaidi na ukuaji wa uzalishaji wa mazao ya kilimo ambao ulikua kwa asilimia 4.7 kwa mwaka 2023. Aidha, ukuaji katika shughuli za ujenzi ulifikia asilimia 3.5 mwaka 2023 ambao ulitokana na uwekezaji unaoendelea kufanyika katika miundombinu. Ukuaji kwa sekta ya madini ulifikia asilimia 11.3 mwaka 2023 uliochangiwa na ongezeko la uzalishaji katika migodi iliyopo hasa dhahabu na uwekezaji mpya katika uchimbaji wa madini.



**(2023)**


*mwaka 2023, pato halisi la taifa lilifikia* ***bilioni 148,399.76***

**5.1%**

**(2023)**

*kiwango cha asilimia cha ukuaji wa pato la taifa*

**Kielelezo Na. 1.5: Mwenendo wa Ukuaji wa Pato la Taifa Mwaka 2018 - 2023**




| | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Q4(Kushoto) | 7.3 | 6.1 | 4.3 | 5.5 | 3.6 | 4.6 |
| Q3(Kushoto) | 7.3 | 8.0 | 5.4 | 5.4 | 5.2 | 5.3 |
| Q2(Kushoto) | 6.0 | 7.6 | 4.4 | 3.8 | 4.7 | 5.2 |
| Q1(Kushoto) | 7.5 | 6.3 | 5.3 | 4.9 | 5.5 | 5.4 |
| Mwaka (Kulia) | 7.0 | 6.9 | 4.5 | 4.8 | 4.7 | 5.1 |

***Chanzo:*** *Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

Viashiria vya uchumi kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2024 vinaonesha uchumi kuendelea kuimarika kutokana na jitihada zinazoendelea za kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi. Aidha, pato la taifa kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2024, lilikua kwa wastani wa asilimia 5.4 ikilinganishwa na asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Hivyo pato la halisi la Taifa linatarajiwa kukua kwa asilimia 5.4 mwaka 2024 na kuongezeka hadi asilimia 5.8 mwaka 2025 na asilimia 6.1 mwaka 2026. Ukuaji huu utategemea utekelezaji endelevu wa miradi mikubwa ya kimkakati inayohusisha miundombinu ya nishati na usafirishaji, jitihada za serikali kuboresha mazingira ya uwekezaji, utekelezaji wa programu ya kuendeleza sekta ya kilimo Awamu ya Pili ASDP II, pamoja na uwekezaji wa Serikali katika sekta za kijamii.


**4.8%** ...........
**(2023)**
*kiwango cha wastani kwa asilimia cha ukuaji wa pato la taifa kimepungua*

**5.4%** ...........
**(2024)**
*kiwango cha wastani kwa asilimia cha ukuaji wa pato la taifa kimeongezeka*

**5.8%** ...........
**(2025)**
*tarajio la kiwango cha wastani kwa asilimia cha ukuaji wa pato la taifa*


**6.1%**
**(2026)**
*tarajio la kiwango cha wastani kwa asilimia cha ukuaji wa pato la taifa*

**Kielelezo Na. 1.6: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi, Kipindi cha Januari hadi Juni kwa Mwaka 2019 –2024**




***Chanzo:*** *Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

**Kielelezo Na. 1.7: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Baadhi ya Shughuli za Kiuchumi (Asilimia) katika kipindi cha Januari hadi Juni kwa Mwaka 2023 na 2024**




***Chanzo:*** *Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

### 2.3.2 Mfumuko wa Bei Nchini

Mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.2 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na asilimia 4.7 kwa mwaka 2022/23, kiwango hiki kipo ndani ya lengo la nchi la asilimia 5.0 na sawia na malengo ya mtangamano wa kiuchumi kikanda (EAC na SADC). Kupungua huko kulitokana na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na bajeti, kupungua kwa bei za baadhi ya bidhaa muhimu zinazoagizwa kutoka nje ya nchi, na utoshelevu wa chakula nchini. Mfumuko wa bei nchini unatarajiwa kubaki ndani ya lengo la nchi la asilimia 5, ukichangiwa na matarajio ya upatikanaji wa chakula cha kutosha nchini, kuimarika kwa upatikanaji wa umeme hususan kukamilika kwa ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere, utulivu wa bei za bidhaa katika soko la dunia pamoja na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na bajeti.

**3.2%**
**(2023/24)**
*kiwango cha mfumuko wa bei nchini*

**4.7%**
**(2022/23)**
*kiwango cha mfumuko wa bei nchini kwa mwaka huo*

### 2.3.3 Sekta ya Nje

**a. Urari wa Malipo ya Nje**

Sekta ya nje imeendelea kuimarika licha ya changamoto mbalimbali zilizoikumba dunia yaani magonjwa, vita na kubadilika kwa sera za nchi zilizoendelea kulikopelekea kuongezeka kwa bei za bidhaa mbalimbali katika soko la dunia. Nakisi ya urari wa malipo ya nje ilipungua kwa asilimia 50.2 na kufikia dola za Marekani milioni 2,469.5 mwaka 2023/24 kutoka dola za Marekani milioni 4,955.6 mwaka 2022/23. Mwenendo huu ulitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi sambamba na kupungua kwa gharama za uagizaji bidhaa na huduma nje ya nchi. Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 14.7 na kufikia dola za Marekani milioni 14,663.9, ikichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu na bidhaa asilia pamoja na mapato ya utalii. Thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ya nchi ilipungua kwa asilimia 5.6 na kufikia dola za Marekani milioni 16,027.0. Mwenendo huu ulitokana na kuimarika kwa uchumi wa dunia, kupungua kwa gharama ya uagizaji wa bidhaa hususan mafuta ya petroli, mitambo, na vifaa vya viwandani pamoja na mbolea na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi. Kupungua kwa nakisi ya malipo ya nje ni ishara nzuri inayoonesha uwezo wa kudhibiti mahitaji ya fedha za kigeni na kujenga akiba ya fedha za kigeni.

**$2,496**
**(2023/24)**
*nakisi ya urari wa malipo ya nje*

**$4,955**
**(2022/23)**
*nakisi ya urari wa malipo ya nje kwa mwaka huo*

**$14,663**
**(2022/23)**
*thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi imeongezeka kwa **14.7%***

b. Akiba ya Fedha za Kigeni

Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Katika kipindi cha mwaka 2023/24, kiwango cha akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,345.5 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,208.3 kipindi kama hicho mwaka 2022/2023. Kiasi hicho kinatosheleza malipo ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4.4, zaidi ya lengo la nchi la kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayokidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi isiyopungua minne.

**(2023/24)**
*kiwango cha akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola **milioni 5,345***

### 2.3.4 Sekta ya Fedha

Katika kipindi cha mwaka 2023/24, Serikali ililenga kuhakikisha ukwasi wa fedha unabaki katika kiwango kinachochagiza ukuaji wa uchumi kwa kutumia mfumo wa ujazi wa fedha ili kuchochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kuhakikisha uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni. Hii inatokana na utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kuongeza ufanisi wa sera ya fedha ili kuendana na mabadiliko ya mazingira ya kiuchumi.

Katika mwaka 2024, Serikali ilianza kutekeleza mfumo wa Riba ya Benki Kuu (Central Bank Rate) kwa kuzingatia maoteo ya mfumuko wa bei na mwenendo wa hali ya uchumi ambapo riba ya Benki Kuu ya asilimia 5.5 katika robo ya kwanza ya mwaka 2024 iliongezeka hadi asilimia 6 kwa kipindi cha mwezi Aprili hadi Julai, 2024 ili kudhibiti athari za kushuka kwa thamani ya shilingi kwenye mfumuko wa bei. Utekelezaji wa sera ya fedha kwa kutumia riba ya Benki Kuu ulikuwa wa kuridhisha na ulifanikiwa kuhakikisha kuwa riba ya siku 7 katika soko la fedha baina ya mabenki inakuwa tulivu, ndani ya wigo usiozidi asilimia 2 chini au juu (+/-2) ya riba ya Benki Kuu.

**a. Viwango vya Riba**

Hadi kufikia Agosti 2024, wastani wa riba katika soko la fedha baina ya mabenki ulifikia asilimia 6.90 ikilinganishwa na asilimia 4.94 kipindi kama hicho mwaka 2023. Aidha, wastani wa riba za dhamana za Serikali ziliongezeka hadi wastani wa asilimia 9.14 mwaka 2023/24 kutoka asilimia 5.73 mwaka 2022/23. Hali hii ilitokana na kupungua kwa ukwasi (tight financial conditions) katika masoko ya fedha, kama ilivyokuwa katika nchi nyingine kufuatia benki kuu duniani kutekeleza sera ya fedha kukabiliana na ongezeko la mfumuko wa bei.

Riba za mikopo zilipungua hadi wastani wa asilimia 15.47 mwaka 2023/24 kutoka asilimia 16.04 mwaka 2022/23. Riba za amana ziliongezeka hadi asilimia 7.32 kutoka asilimia 7.16 mwaka 2022/23. Riba za mikopo kwa sekta binafsi zinatarajiwa kupungua kutokana na hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha sekta ya fedha pamoja na matarajio ya kuwa na mfumuko wa bei mdogo nchini.

**b. Mikopo kwa Sekta Binafsi**

Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 18.1 katika mwaka 2023/24 ikilinganishwa na asilimia 22.2 mwaka 2022/23. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na mikopo iliyoelekezwa kwenye kilimo, uchimbaji madini, usafirishaji na mawasiliano, shughuli binafsi na uzalishaji viwandani.

Aidha, mikopo kwa sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 39.5, kutokana na matokeo ya hatua za kisera zilizolenga kushusha viwango vya riba pamoja na juhudi za Serikali kuongeza bajeti katika sekta ya kilimo. Vilevile, mikopo katika sekta ya viwanda na uzalishaji ulikua kwa asilimia 25.7, usafirishaji na mawasiliano (asilimia 20.7), ujenzi (asilimia 18.0) na shughuli binafsi (asilimia 16.4).

Matokeo hayo yanaonesha mwelekeo chanya katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya sekta mbalimbali nchini. Ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi, hususan katika sekta za kilimo, viwanda na uzalishaji, na uchimbaji madini, linaashiria

uimarishaji wa mazingira ya biashara na ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Hatua za kisera zilizolenga kupunguza viwango vya riba na kuongeza bajeti katika sekta muhimu kama kilimo zimeonekana kuwa na matokeo chanya katika kuchochea ukuaji huo.

**c. Ukwasi na Faida za Biashara katika Benki**

Benki za biashara zimeendelea kuimarika na kutengeneza faida zikiwa na viwango vya kutosha vya mitaji na ukwasi, ambapo kwa mwaka 2023/24 faida ya benki za biashara ilikuwa shilingi bilioni 1,060.87. Aidha, mikopo chechefu ilipungua hadi asilimia 4.1 kutoka asilimia 5.3 mwaka 2022/23. Uwiano wa mtaji wa msingi kwa rasilimali zote ulifikia asilimia 18.9 mwezi Agosti 2024, ikilinganishwa na kiwango kinachokubalika kisheria cha asilimia 10. Aidha, uwiano wa ukwasi wa sekta ya benki kiujumla (Liquid Assets to Demand Liabilities) ulikuwa asilimia 27.7 mwezi Agosti 2024 ikilinganishwa na asilimia 25.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Uwiano huu ulikuwa juu ya kiwango cha chini kinachokubalika kisheria cha angalau asilimia 20 na hivyo kuendelea kuwa toshelevu kwa mahitaji ya shughuli mbalimbali za kiuchumi.

### 2.3.5 Deni la Serikali

Hadi mwezi Juni 2024, deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 96,884.18. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 31,951.24 na deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 64,932.94. Fedha hizo zilielekezwa katika kugharamia miradi ya maendeleo, ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme na maji.

Mwaka 2023/24 kampuni za Fitch Ratings na Moody’s Investors Service zilifanya mapitio ya tathmini ya nchi kukopesheka katika masoko ya mitaji ya kimataifa na kuchapisha matokeo ya daraja B1 na B+ mtawalia. Matokeo mazuri ya tathmini hizo yalitokana na ukuaji mzuri wa uchumi unaoweza kuhimili mitikisiko ya kiuchumi, utekelezaji wa mageuzi ya kimuundo yanayoboresha mazingira ya biashara, ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa fedha za umma.

Matokeo hayo yatawezesha kupungua kwa gharama za mikopo (riba za mikopo) kutokana na kuongezeka kwa imani kwa wakopeshaji na hivyo kuwezesha ugharamiaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo; kuongezeka kwa uwekezaji kutoka nje ya nchi ambao utasaidia kukuza uchumi.


### 2.3.6 Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu

#### *2.3.6.1 Hali ya Umaskini*

Mwaka 2023, Serikali iliendelea kutekeleza sera, programu na miradi mbalimbali yenye lengo la kupunguza umaskini na kuchochea maendeleo ya watu. Jitihada hizo zinaongozwa na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wenye dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Kutokana na utafiti wa mapato na matumizi ya Kaya Binafsi wa 2017/18, taarifa ya hali ya umaskini nchini inaonesha kuwa, umaskini wa mahitaji ya msingi umepungua kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/12 hadi asilimia 26.4 mwaka 2017/18 na kiwango cha umaskini wa chakula kimepungua kutoka asilimia 9.7 mwaka 2011/12 hadi asilimia 8.0 mwaka

2017/18. Aidha, kutokana na makadirio ya hali ya umaskini yanayofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, hali ya umaskini inakadiriwa kupungua hadi asilimia 25.7 mwaka 2020 na umaskini wa chakula inakadiriwa kupungua hadi asilimia 7.3 mwaka 2020.

Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuboresha ustawi wa jamii na kupunguza umaskini uliokithiri kwa kufanya yafuatayo: kuwezesha upatikanaji wa ajira 875,633 kutokana na utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati; kuwezesha upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu kiasi cha shilingi 3,197,403,492 kwa kampuni 1,148 zilizonufaisha vijana 164,443 katika Halmshauri 46 kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana; kutoa mikopo ya shilingi bilioni 30.9 kwa vikundi 5,120 vya wanawake wajasiriamali katika Halmashauri zote nchini kupitia utaratibu wa kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani; kuanzisha programu mbalimbali ikiwemo Jenga Kesho Iliyobora katika sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi); kutenga ekari 491,929 katika Halmashauri 176 ambazo zimenufaisha vijana 193,053; kuendelea kutekeleza programu ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini – TASAF ambapo hadi Desemba 2023, kaya zinazonufaika na Mpango huu zilikuwa 1,371,916 zenye wanufaika 6,938,481 ikilinganishwa na kaya 1,371,038 zenye wanufaika 6,596,820 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na marekebisho ya taarifa kwa baadhi ya kaya zilizokuwa kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya tathmini ya Mpango. Kati ya wanufaika wa Mpango, wanawake walikuwa 3,600,267 (asilimia 51.9) na wanaume 3,338,214 (asilimia 48.1). Hata hivyo, Serikali imeendelea kupeleka huduma za msingi karibu na wananchi hususan huduma za maji, elimu, afya pamoja na miundombinu ya nishati na barabara ili kumpunguzia mwananchi gharama za maisha na kupunguza umaskini.




Lengo la hatua hizi ni kuwezesha kufikia shabaha zilizoanishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ya kupunguza umaskini kwa asilimia 22.0 na asilimia 5.8 kwa kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi na chakula mtawalia.

**25.7%**
**(2020)**
*kiwango cha hali ya umaskini kimepungua*

**7.3%**
**(2020)**
*kiwango cha umaskini wa chakula kimepungua*

**875,633**
*upatikanaji wa ajira umeongezeka*

*upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu ya thamani **bilioni 3.1***

**1,148**
*idadi ya makampuni yaliyonufaika na mkopo*

**491,926**
*ekari zilizotengwa katika halmashauri 176*

#### *2.3.6.2 Maendeleo ya Watu*

Serikali imeendelea na jitihada za kuboresha maendeleo ya watu kwa lengo la kuimarisha maisha ya watu ili kufikia matamanio yaliyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Juhudi hizo ni pamoja na: kuendelea kutoa elimu bila ada; kuendelea kuboresha upatikanaji wa maji mijini na vijijini; kuendelea kuboresha ushiriki wa sekta binafsi katika kutoa huduma za afya hususan maeneo ya vijijini; kuendelea na ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali; na kuendelea na ujenzi wa barabara za kufungua fursa za kiuchumi katika maeneo ya mijini na vijijini. Kutokana na utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo, kumekua na matokeo chanya katika viashiria vya maendeleo ya watu ikiwemo:

i. Kuongezeka kwa wastani wa umri wa kuishi kutoka miaka 66.1 mwaka 2019 hadi miaka 68.3 (2023/2024) na makadirio ya kufikia miaka 68.0 kwa mwaka 2025. Aidha, wastani wa umri wa kuishi kwa kuzingatia jinsia, unakadiriwa kufikia miaka 70.4 kwa wanawake na miaka 65.5 kwa wanaume mwaka 2024;

ii. Vifo vya watoto wa umri chini ya miaka mitano vimepungua kutoka vifo 81 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2019/20 hadi kufikia vifo 43 kwa vizazi hai 1000 mwaka 2022;

iii. Kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 454 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2019/20 hadi vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022;

iv. Idadi ya watanzania wanaotumia huduma ya bima imeongezeka kutoka asilimia 9 mwaka 2019/20 na kufikia asilimia 15.3 ambapo asilimia 8 ni wanatumia NHIF, asilimia 0.3 wanatumia NSSF, asilimia 6 wanatumia ICHF na asilimia moja wanatumia bima za afya zinazotolewa na sekta binafsi;

v. Kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya awali kutoka wanafunzi 1,377,409 mwaka 2019/20 hadi wanafunzi 1,679,559 mwaka 2023/24;

vi. Kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya msingi kutoka wanafunzi 10,925,896 mwaka 2019/20 hadi wanafunzi 11,391,185 mwaka 2023/24;

vii. Kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya sekondari kutoka wanafunzi 2,473,506 mwaka 2019/20 hadi 3,314,198 mwaka 2023/24;

viii. Kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa vijijini kutoka wastani wa asilimia 70 mwaka 2019/20 hadi asilimia 79.6 Desemba 2023 ikiwa na lengo la kufikia asilimia 85 mwaka 2025/26. Kwa upande wa maeneo ya mijini, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama imeongezeka kutoka wastani wa asilimia 84 mwaka 2019/20 hadi wastani wa asilimia 90, Desemba 2023 ikiwa ni lengo la kufikia asilimia 95 ifikapo mwaka 2025/26; na

ix. Kuunganishwa na huduma ya umeme kwa jumla ya vijiji 9,112 kati ya vijiji 12,345 vya Tanzania Bara mwaka 2019/20 ikilinganishwa na jumla ya vijiji 12,167 vilivyounganishwa mwaka 2023/24 ikiwa ni lengo la kuunganisha vijiji vyote nchini ifikapo mwaka 2025/26.

#### *2.3.6.3 Idadi ya Watu*

Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, imeonesha kuwa idadi ya watu Tanzania imeendelea kuongezeka kutoka watu 44,928,923 mwaka 2012 hadi watu 61,741,120 mwaka 2022. Ukuaji huo unatarajiwa kuendelea kuongezeka kutokana na ongezeko la wastani wa asilimia 3.2 ambapo inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2035 idadi ya watu nchini itakuwa 87,509,630. Hata hivyo, ongezeko hili haliendani sawa na kasi ya ukuaji wa uchumi ambao bado unakua kwa wastani wa asilimia kati ya 5 – 6 kila mwaka tofauti na kiwango kinachopendekezwa cha asilimia 8 hadi 10 ili kupunguza kiwango cha umaskini. Pamoja na uwepo wa hali hiyo, nchi yetu ni miongoni mwa nchi Barani Afrika ambazo zina fursa ya kutumia faida zitokanazo na matumizi mazuri ya idadi ya watu (demographic dividend). Fursa hizo ni pamoja na uwepo wa kundi kubwa la vijana wenye umri wa miaka 15-35 (youth bulge) wapatao 21,312,411 kwa Tanzania (Wanaume 10,159,205 (33.8%) na wanawake 11,153,206 (35.2%) kwa Tanzania sawa na asilimia 34.5 ya idadi ya watu. Aidha, kwa Tanzania Bara ni 20,612,566 sawa na asilimia 34.4 (Wanaume 9,827,426 (33.7%) na wanawake 10,785,140 (35.1%) mwaka 2022 ikienda sawa na maoteo ya Afrika ya kuwa na asilimia 42 ya vijana wote duniani ifikapo mwaka 2030. Fursa nyingine ni pamoja na uwiano mzuri wa idadi ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi wa asilimia 53.4 ya idadi ya watu wote nchini; na uwepo wa msukumo kitaifa wa matumizi ya takwimu za idadi ya watu katika mipango.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia imeendelea kuwekeza katika rasilimali watu hususan elimu na ujuzi ili kuhakikisha rasilimali hii inayokuwa kwa kasi hususan vijana inakuwa bora na inayokidhi matakwa ya wakati ambayo yanatawaliwa na teknolojia na ubunifu na yenye fikra za kimageuzi katika kuleta maendeleo. Vile vile, juhudi zinaendelea kuwekwa katika kuhakikisha watoto wanapata lishe bora, huduma za chanjo kuanzia umri mdogo kwa ajili ya kutokomeza udumavu ambao unaathiri ubora wa idadi ya watu katika Taifa .

## 2.4 Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025/26

Kwa kuzingatia mapitio ya hali ya uchumi kama ilivyoanishwa katika sehemu 2.2, lengo kuu la Serikali katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/26 litakuwa kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, kupanua wigo wa ujumuishi katika shughuli za uchumi, kuongeza kasi ya mageuzi ya uchumi na kuondoa umaskini, kutekeleza mikakati ya kuongeza mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi ili kuongeza mapato ya fedha za kigeni na kuweka mkazo kwenye shughuli za uchumi zinazozalisha ajira kwa wingi na kuchochea ustawi kwa watanzania wote.

### 2.4.1 Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi Jumla

Malengo na shabaha za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:


i. Pato Halisi la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 5.4 mwaka 2024 na kuongezeka hadi asilimia 5.8 mwaka 2025 na asilimia 6.1 mwaka 2026;
ii. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja wa wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati;
iii. Mapato ya ndani kufikia asilimia 16.1 na mapato ya kodi asilimia 13.0 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2025/26; na
iv. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

### 2.4.2 Misingi (Assumptions) ya Mpango kwa Mwaka 2025/26

Mafanikio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 yamejegwa katika misingi ifuatayo:

i. Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama na utulivu wa ndani ya nchi na katika nchi jirani;
ii. Kuendelea kudumisha utawala bora na utawala wa sheria nchini;
iii. Kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini;
iv. Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za uwekezaji na biashara;
v. Kuendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili (ukame, vita, magonjwa ya mlipuko na mafuriko);
vi. Kuwa na nidhamu katika utekelezaji wa mpango na bajeti;
vii. Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa; na
viii. Kuendelea kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

# SURA YA TATU





# MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO

## 3.1 Utangulizi

Mipango ya maendeleo ya Tanzania yanaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Pamoja na hatua nyingine, Dira hii inalenga kuona Tanzania inafuzu kuingia katika kundi la nchi za uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 na kuwa na kiwango cha juu cha maendeleo ya watu. Katika kufikia Dira hii, Serikali imekuwa ikitekeleza Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano. Kwa sasa Serikali inatekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wenye maeneo ya vipaumbele vitano. Vipaumbele hivyo ni kuchochea uchumi shirikishi na shindani; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza uwekezaji na biashara; kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza rasilimali watu. Sura hii inaeleza hatua zilizochukuliwa na matokeo ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi ya kielelezo na ile ya kimkakati katika mwaka 2023/24.

## 3.2 Utekelezaji wa Vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano katika Mwaka 2023/24 na Utekelezaji katika Kipindi cha Robo ya Kwanza Mwaka 2024/25

### 3.2.1 Miradi ya Kielelezo

Serikali imepanga kutekeleza miradi 17 ya kielelezo inayolenga kuleta matokeo katika maeneo matano ya kipaumbele ya Mpango wa

Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, ambayo ni uchumi shirikishi na shindani; kuongeza uzalishaji viwandani; kuvutia uwekezaji na biashara; maendeleo ya watu; na kuendeleza rasilimali watu. Utekelezaji wa miradi ya kielelezo upo katika hatua mbalimbali. Kati ya miradi hiyo, kuna ambayo ipo katika hatua za juu za utekelezaji (kwa sehemu imeanza kutumika), miradi inayoendelea na ambayo ipo katika hatua za awali. Kwa sehemu kubwa miradi ya kielelezo ni ya miundombinu ya usafiri na usafirishaji na nishati. Aidha, miradi ya miundombinu ya TEHAMA imeelezewa chini ya miradi ya kimkakati ya kisekta.

#### *3.2.1.1 Miundombinu ya Usafirishaji*

Miradi hii ni ile inayohusiana na ujenzi na huduma za usafirishaji ikiwemo barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege. Katika eneo hili Serikali ilipanga kutekeleza miradi ifuatayo:

i. **Ujenzi wa Madaraja Makubwa ya Juu**

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano uliainisha ujenzi wa madaraja makubwa ya juu ambayo ujenzi wake utachochea shughuli za kiuchumi na kurahisisha usafiri na usafirishaji ili kupunguza msongamano mijini na kuunganisha Tanzania na nchi jirani za DRC, Uganda, Rwanda na Burundi. Madaraja haya ni Kigongo - Busisi pamoja na madaraja ya juu jijini Dar es salaam. Baadhi ya miradi imekamilika na mingine inaendelea katika hatua mbalimbali. Aidha, mradi wa Kigongo – Busisi umefikia asilimia 92.15 ambapo ukikamilika utachochea ukuaji wa uchumi kwa ujumla na kurahisisha usafirishaji wa bidhaa zinazotoka na kwenda nchi jirani. Kukamilika kwa madaraja haya kutaongeza ufanisi katika shughuli za kiuchumi, kukuza biashara na kuvutia uwekezaji.

ii. **Ujenzi wa Reli ya Kisasa kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR)**

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kujenga reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa ili kuinua na kuimarisha usafirishaji wa bidhaa na usafiri ndani ya nchi pamoja na kuunganisha Tanzania na mitandao ya usafirishaji wa nchi jirani. Mpango pia ulilenga kuanza ujenzi wa reli ya kusini kwa kiwango cha kimataifa na kuiunganisha na reli ya TAZARA.

Hadi kufikia Septemba 2024, ulazaji wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa umefikia kilometa 625.84, ikilinganishwa na lengo la kilometa 1,219 mwaka 2025/26 ambapo ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (asilimia 99.27), Morogoro – Makutupora (asilimia 97.14), Makutupora – Tabora (asilimia 14.53), Tabora –Isaka (asilimia 6.08), Isaka – Mwanza (asilimia 60.28) na Tabora – Kigoma (asilimia 6.48). Aidha, huduma za usafirishaji wa abiria kutoka Dar es Saalam hadi Dodoma imeanza ambapo hadi Agosti 2024, abiria 420,301 wamesafirishwa na hivyo, kupunguza muda wa kusafiri na kuongeza fursa ya usafiri mbadala. Hii imechangia kuongeza tija katika uchumi na biashara. Vile vile, ujenzi wa mradi wa SGR umechangia Tanzania kuwa nchi ya 58 mwaka 2023/24 kutoka nafasi ya 83 mwaka 2019/20 kwa ubora wa reli duniani, jambo ambalo ni muhimu katika ushindani wa biashara wa kikanda na kimataifa. Aidha ujenzi wa reli ya kusini upo katika hatua za awali za uchambuzi na majadiliano.

**Septemba, 2024**
**km 625.84** *umbali wa ulazaji wa reli ya kati kiwango cha mataifa*

**Agosti, 2024**
**420,301** *idadi ya Abiria wanaosafiri kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma*

### iii. Ununuzi wa Meli na Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kujenga bandari ya uvuvi na kununua meli za uvuvi kwa lengo la kukuza soko la ndani na kimataifa la mazao ya uvuvi. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imeendelea na ujenzi wa Bandari ya uvuvi katika eneo la Kilwa Masoko ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 71. Aidha, katika mradi wa ununuzi wa meli hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa Upembuzi Yakinifu wa uendeshaji wa meli za uvuvi. Utekelezaji wa mradi huu utaongeza uvunaji wa rasilimali za bahari; kuongeza mazao ya samaki katika soko la ndani na nje. Hii itapelekea kuongeza lishe bora, kipato na kupunguza umaskini kwa jamii na wavuvi wadogo wadogo.


#### *3.2.1.2 Kuboresha Shirika la Ndege*

Katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali ilipanga kuimarisha uendeshaji wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) na kununua ndege mpya ili kufikisha idadi ya ndege 19 ifikapo 2025/26; kutoa mafunzo kwa marubani na wahandisi; na kuboresha miundombinu ya karakana. Uboreshaji wa huduma za Shirika la Ndege unatarajiwa kuchochea uwekezaji katika sekta za utalii na usafirishaji. Kufikia mwaka 2023/24 jumla ya ndege 16 zimenunuliwa sawa na asilimia 84.2 ya lengo ifikapo 2025/26. Huduma ya uhakika ya usafiri wa anga, pamoja na masuala mengine, umechangia ongezeko la watalii wa ndani na nje ya nchi, hivyo kuchangia ongezeko na mchango wa sekta ya utalii katika uchumi wa Tanzania. Vilevile usafirishaji wa mazao na bidhaa za kilimo umeongezeka kutokana na uwepo wa ndege kubwa ya mizigo hivyo kuchochea ongezeko la mapato yatokanayo na sekta hiyo hususan sekta ndogo ya mbogamboga na matunda.

#### *3.2.1.3 Miundombinu ya Nishati*

Miundombinu ya nishati ina mchango mkubwa katika kufikia matokeo tarajiwa ya maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Kutokana na umuhimu huo, Mpango ulilenga kutekeleza miradi nane (8) ya kielelezo ya nishati inayojumuisha umeme wa maji, gesi, makaa ya mawe, na bomba la kusafirisha mafuta ghafi. Miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Kwa upande wa miradi ya kuzalisha umeme kwa njia ya maji, miradi iliyopangwa kutekelezwa ni mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere (MW 2,115), Ruhidji (MW 358) na Rumakali (MW 222). Kati ya hiyo, utekelezaji wa mradi wa Julius Nyerere (MW 2,115) umefikia asimia 99.21 hadi mwezi Septemba, 2024 na kuanza uzalishaji wa MW 740 zilizoingizwa katika Gridi ya Taifa. Miradi miwili iliyobaki ipo katika hatua za maandalizi ya utekelezaji.



**2018 - 2024**
**MW 2,115**
*mradi wa Julius Nyerere utekelezaji wake umefikia **99.21%***

Kwa upande wa miradi ya mafuta na gesi asilia, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kujenga mradi wa kusindika gesi asilia kuwa kimiminika (LNG) mkoani Lindi, na utafutaji wa mafuta na gesi katika vitalu vya Eyasi - Wembere na Mnazi Bay. Miradi yote mitatu ya mafuta na gesi ipo katika hatua za maandalizi. Miradi hii itakapokamilika itachangia katika ukuaji wa uchumi, kuongeza fedha za kigeni, fursa za ajira na huduma za ugavi na biashara.

Kwa upande wa ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi lenye urefu wa km 1,443 kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania), Serikali imelipa fidia kwa asilimia 99.2 kwa wananchi waliopisha utekelezaji wa mradi, kukamilisha ujenzi wa karakana, makambi na vituo vya kuhifadhi mabomba, kuwasili nchini mabomba ya kuwezesha kujenga kilomita 700 kwa kuwekewa mfumo wa kuhifadhi joto na kuendelea na ujenzi wa kituo cha kupokelea na kuhifadhi mafuta. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza ajira, mapato ya Serikali na kuhamasisha shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi. Matokeo haya yote yataongeza chachu ya ukuaji wa uchumi shindani na endelevu.

**km 1,443**

*urefu wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima hadi Tanga*

Mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma na chuma Liganga umelenga kuzalisha makaa ya mawe, chuma, chuma cha pua na madini mengine yatakayoongeza uzalishaji wa umeme na kuchangia katika ajenda ya mageuzi ya viwanda na ushindani wa bidhaa. Utekelezaji wa miradi hiyo yenye uhusiano wa moja kwa moja na sekta ya madini, nishati na kilimo upo katika hatua za awali ambapo ulipaji wa fidia umefanyika na majadiliano na wawekezaji yanaendelea.

#### *3.2.1.4 Miradi ya Kuongeza Uzalishaji Viwandani*

Serikali kupitia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano iliainisha miradi mitatu ya kielelezo yenye kujielekeza moja kwa moja kwenye kuongeza uzalishaji viwandani. Miradi hiyo ni Magadi soda (Engaruka), kiwanda cha sukari Mkulazi na Kanda maalum za uchumi na uwekezaji.

**i. Mradi wa Magadi Soda**

Mradi wa Magadi soda upo katika hatua za majadiliano kati ya Serikali na mwekezaji. Mradi huu utakapokamilika utaongeza ajira; utapunguza matumizi ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza magadi soda kutoka nchi za nje; kuongeza malighafi kwenye sekta za madini, viwanda na kilimo pamoja na fursa ya ukuaji wa biashara na kuongeza mauzo nje ya nchi. Hivyo, mradi huu utanufaisha wananchi moja kwa moja na kupitia huduma wezeshi zitakazopatikana baada ya mradi kukamilika.

**ii. Kiwanda cha Sukari Mkulazi**

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuongeza upatikanaji wa sukari nchini kwa kujenga kiwanda chenye uwezo wa kuzalisha tani 250,000 za sukari kwa mwaka na kuzalisha fursa za ajira 100,000.

Ili kufikia lengo hilo, kiwanda cha sukari Mkulazi kimelenga kuongeza upatikanaji wa sukari nchini kwa kuzalisha tani 50,000 za sukari kwa mwaka na kuzalisha fursa za ajira zinazofikia 11,315. Baada ya miaka mitano ya kwanza ya uzalishaji, Kampuni inakusudia kuongeza uzalishaji wa sukari kutoka tani 50,000 hadi tani 75,000 kwa mwaka.

Aidha, kati ya tarehe 15 Desemba, 2023 hadi tarehe 24 Machi, 2024, kiwanda kilianza uzalishaji wa majaribio wa sukari ya matumizi ya majumbani “brown sugar”. Uzalishaji rasmi wa sukari ya kibiashara ulianza tarehe 1 Julai, 2024 ambapo hadi

kufikia tarehe 30 Septemba 2024 jumla ya tani 15,051 za sukari zimezalishwa kwa ajili ya matumizi ya majumbani. Kuanza kwa uzalishaji wa sukari katika kiwanda cha Mkulazi kutasaidia kupunguza tatizo la uhaba wa sukari nchini na kuchangia kuongeza ajira nchini.

#### iii. Kanda Maalum za Uchumi na Uwekezaji

Eneo hili linahusisha aina mbili ya miradi, ambazo ni kanda maalum za kiuchumi, Bagamoyo na eneo la Benjamin Mkapa; na maeneo mawili maalum ya uwekezaji ambayo ni bandari huru ya Mtwara na eneo maalum la uwekezaji Manyara.

Katika eneo la miradi ya kanda maalum za uchumi na uwekezaji, Serikali kupitia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ililenga kuendelea kuimarisha miundombinu katika kanda hizo na kuanzisha maeneo mengine mapya katika mikoa ya Singida (Manyoni), Pwani, Kigoma, Tanga, Manyara, Mara, na Ruvuma. Serikali imetenga maeneo 17 kwa ajili ya kuanzisha kanda maalum za uwekezaji ambapo maeneo mawili ya Benjamin William Mkapa SEZ na Mtwara yameanza uzalishaji, na maeneo 15 yapo katika hatua mbalimbali za uendelezaji. Utekelezaji wa miradi katika kanda hizi maalum utaongeza idadi na thamani ya uwekezaji na kongani za uwekezaji, ajira, uzalishaji, fedha za kigeni na huduma. Kukamilika kwa miradi hii kutaongeza ushindani katika soko la ndani na nje, uzalishaji viwandani na kuvutia uwekezaji nchini.

### 3.2.2 Programu na Miradi ya Kimkakati ya Kisekta

Programu na miradi ya kimkakati katika sekta zote zina uhusiano wa moja kwa moja na usio wa moja kwa moja na matokeo ya maeneo matano (5) ya vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) na utekelezaji wake umekuwa na mchango mkubwa katika kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Utekelezaji wa programu na miradi ya kimkakati ya kisekta na mchango wake katika kufikia matokeo tarajiwa ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni kama ifuatavyo:

#### *3.2.2.1 Sekta ya Ujenzi*

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano,sekta ya ujenzi imekua na kuongeza mchango wake katika Pato la Taifa. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango, mtandao wa barabara zinazopitika wakati wote za kitaifa na mikoa umeongezeka na kufikia kilometa 37,225.75 mwaka 2023/24 kutoka kilometa 32074.99 mwaka 2021/22 ambazo zimerahisisha usafirishaji wa bidhaa na hivyo kupunguza kasi ya upandaji wa bei sokoni na kuchangia ushindani wa kibiashara katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Kuongezeka kwa mtandao wa barabara pia kumechangia uzalishaji viwandani kwa kuhakikisha upatikanaji wa malighafi za viwandani kwa wakati na kwa gharama nafuu na kuchochea uwekezaji na biashara. Aidha, kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika ujenzi wa vivuko vya Serikali na vya biashara kumechangia ongezeko la ajira, kipato, kuchochea uchumi na kujenga uwezo wa sekta binafsi ya ndani. Vile vile, maboresho katika taasisi za usimamizi na hatua nyingine katika sekta ya ujenzi yamechangia katika kukuza ujuzi wa wakandarasi hivyo kuleta ujuzi kwa wataalamu wa ndani na uwezo wa kutumia teknolojia kutoka nje ya nchi.

**Jedwali 3.1: Viashiria na Shabaha za Utekelezaji katika Sekta ya Ujenzi**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Miundombinu (Nafasi katika mpangilio, kati ya nchi 189 kimataifa | | | | 60 | 55 | 50 | 45 |
| 2. | Kiwango cha wastani wa ukuaji (%) | 9.0 | 14.1 | 14.0 | 14.1 | | 9.9 | 9.9 |
| 3. | Mchango katika Pato la Taifa (%) | 14.8 | 14.3 | 13.8 | 14 | 14.1 | 16.7 | 16.7 |
| 4. | Mchango wa Kampuni za Ndani katika Soko la Ujenzi (%) | 35 | 35 | 35 | 35 | 35 | 40 | 60 |
| 5. | Idadi ya Ajira zilizozalishwa katika Miradi ya Maendeleo | 23,585 | 11,862 | 24,007 | 47,617 | 26,367 | 30,129 | 30,155 |
| 6. | Nafasi ya barabara katika mpangilio wa kimataifa | 86 | | | 42 | 39 | 27 | 26 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Ujenzi*

### *3.2.2.2 Sekta ya Uchukuzi*

Miradi ya kimkakati katika sekta ya uchukuzi, inachangia kwa kiasi kikubwa katika matokeo ya vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Matokeo ya utekelezaji wa afua nyingi za sekta ya uchukuzi yameelezwa katika miradi ya kielelezo ikiwemo ujenzi wa reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa.

Utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya sekta ya uchukuzi imewezesha kuongeza kiasi cha abiria wanaosafirishwa na reli kutoka 972,000 mwaka 2019/20 kufikia abiria 1,213,225 mwaka 2023/24, kuongezeka kwa idadi ya meli zilizohudumiwa na bandari kutoka meli 3,704 mwaka 2019/20 hadi meli 4,487 mwaka 2023/24. Hii imesaidia kurahisisha biashara ndani na nje ya nchi hivyo kuongeza ushindani katika masoko ya kikanda na kimataifa na kuchochea maendeleo ya viwanda

**Jedwali 3.2 Viashiria na Shabaha za Utekelezaji katika Sekta ya Uchukuzi**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Nafasi ya reli katika mpangilio wa kidunia | 83 | 83 | 83 | 78 | 58 | 63 | 70 |
| 2. | Urefu wa reli ya kati ya mwendo-kasi (SGR) kwa kilometa | 395.2 | 451.43 | 487.9 | 553.03 | 625.84 | 1,219 | 1,219 |
| 3. | Kiasi cha shehena kinachosafirishwa na reli (tani) | 1,569,536 | 805,433 | 842,651 | 723,609 | 600,502 | 1,272,682 | 2,162,258 |
| 4. | Idadi ya abiria wanaosafirishwa na reli | 972,000 | 1,250,373 | 1,143,787 | 1,394,058 | 1,213,225 | 2,505,523 | 2,272,682 |
| 5. | Nafasi ya bandari katika mpangilio wa kidunia | 361 | 361 | 361 | 312 | 312 | N/A | 50 |
| 6. | Muda wa meli kurejea kituoni kwake (siku) | 9.5 | 8.8 | 9.7 | 8.7 | Wastani 13.1 | 3 | 2 |
| 7. | Idadi ya meli zinazoingia bandarini kwa mwezi | 281 | 353 | 391 | 473 | 374 | 491 | 254 |
| 8. | Muda wa makasha kukaa bandarini (siku) | 7 | | | 9.2 | 6.7 | 6 | 5 |
| 9. | Muda wa meli kukaa bandarini (siku) | 3.7 | 3.7 | 4.6 | 4.4 | 4.1 | 6 | 2 |
| 10. | Idadi ya bandari kavu | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 3 | 3 |
| 11. | Idadi ya meli zinazohudumiwa | 3,704 | 4,241 | 4,686 | 5,675 | 4,487 | 4,500 | 4,000 |
| 12. | Mizigo inayotoka nje kuelekea nchi za jirani (tani milioni) | 3,506,732 | 3,515,142 | 5,070,972 | 5,672,659 | 6,150,130 | 10,000,000 | 18,000,000 |
| 13. | Mizigo ya kwenda nje toka kwa nchi jirani (tani milioni) | 2,059,510 | 2,064,448 | 2,730,523 | 2,686,461 | 3,036,981 | 10,000,000 | 10,000,000 |
| 14. | Idadi ya ndege zilizonunuliwa | 11 | 11 | 11 | 13 | 16 | 17 | 19 |
| 15. | Idadi ya ndege za mizigo zilizonunuliwa | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 1 |

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 16. | Idadi ya ndege za abiria za masafa marefu zilizonunuliwa | 2 | 2 | 2 | 4 | 6 | 4 | 3 |
| 17. | Idadi ya ndege za abiria za masafa ya kati (kanda) zilizonunuliwa | 2 | 2 | 2 | 6 | 8 | 8 | 8 |
| 18. | Idadi ya ndege za ATCL zinazofanya kazi | 10 | 10 | 12 | 13 | 15 | 17 | 19 |
| 19. | Idadi ya wanaanga waliofunzwa | 61 | 99 | 279 | 320 | 567 | 1,359 | 1,359 |
| 20. | Idadi ya Viwanja vya ndege vyenye mifumo ya usimamizi wa taarifa za viwanja vya ndege (AMIS) | 1 | 1 | 1 | 1 | 2 | 6 | 14 |
| 21. | Idadi ya mitambo ya ulinzi kwenye viwanja vya ndege (X-ray machines) | 46 | 80 | 83 | 83 | 85 | 87 | 71 |
| 22. | Viwanja vya ndege vyenye uzio kuzunguka kiwanja | 9 | 9 | 11 | 16 | 16 | 21 | 27 |
| 23. | Idadi ya rada za hali ya hewa zilizonunuliwa | 5 | 7 | 7 | 7 | 7 | 5 | 7 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Uchukuzi*

### *3.2.2.3 Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari*

Miradi katika sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ililenga kuongeza matumizi ya mtandao wa intaneti ili kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, unaonesha kuwa watumiaji wa mtandao wa intaneti wameongezeka kufikia asilimia 61.2 mwaka 2023/24 kutoka asilimia 52.1 mwaka 2021/22 na hivyo, kuchangia ongezeko la biashara kupitia mitandao na kupunguza gharama na upatikanaji wa taarifa za uzalishaji, masoko na huduma. Aidha, kuunganisha mkongo wa taifa wa mawasiliano na nchi jirani ikiwemo Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia na Msumbiji kumerahisisha ufanyaji wa biashara kati ya Tanzania na nchi hizo, hatua inayokuza uchumi wa kidigitali. Vilevile, zaidi ya majengo 18,186,000 nchini yana anwani za makazi, jambo ambalo linatarajiwa kuwa na manufaa kibiashara na huduma. Hatua hizi kwa ujumla wake zinachangia matokeo katika vipaumbele vya kuchochea ushindani, uzalishaji viwandani na uwekezaji na biashara.

**Jedwali 3.3: Viashiria na Shabaha za Utekelezaji katika Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| **Sekta ya Mawasiliano** | | | | | | | | |
| 1. | Uwiano wa watumiaji wa intaneti nchini (%) | 43 | 52.1 | 50.7 | 54.5 | 61.2 | 75 | 80 |
| 2. | Mchango wa Sekta ya Mawasiliano katika Pato la Taifa (%). | 1.5 | 1.5 | 1.5 | 1.5 | 1.5 | 1.5 | 3 |
| 3. | Idadi ya watu wanaomiliki simu za mkononi (milioni). | 25.1 | | | | 39 | | 45 |
| 4. | Idadi ya Majengo yenye Anwani za Makazi | - | - | - | 18,000,000 | 18,000,000 | 18,186,000 | 18,250,000 |
| 5. | Idadi ya Anwani zilizosajiliwa kwenye Mfumo wa Anwani za Makazi | - | - | - | 12,385,956 | 12, 891,392 | 13,200,000 | 15,231,392 |
| 6. | Idadi ya Huduma zilizosajiliwa kwenye Mfumo wa Anwani za Makazi | - | - | - | 800,000 | 831,436 | 1,000,000 | 1,100,000 |
| 7. | Idadi ya Barua za Utambulisho zilizotolewa kupitia Mfumo wa Kidijitali wa Anwani za Makazi | - | - | - | 800 | 848 | 15,000 | 15,500 |
| **Sekta ya Habari** | | | | | | | | |
| 1. | Idadi ya Halmashauri za wilaya zinazofikiwa na matangazo ya TBC (TBCFM na TBCTaifa). | 102 | 119 | 134 | 137 | 148 | 158 | 161 |
| 2. | Idadi ya magazeti yanayozalishwa na Shirika la Magazeti la Taifa (TSN). | 1,334,568 | 1,787,309 | 1,543,460 | 1,509,135 | 2,934,000 | 5,198,387 | 6,707,522 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari*

### *3.2.2.4 Sekta ya Nishati*

Sekta ya Nishati ni wezeshi katika kuchagiza na kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii. Shughuli za kiuchumi na kijamii zinazotegemea sekta ya nishati ni pamoja na usafiri na usafirishaji, biashara na uwekezaji, uzalishaji viwandani na huduma. Mafanikio na matokeo ya utekelezaji wa miradi ya nishati yameelezwa katika miradi ya kielelezo ikiwemo Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyere (JNHPP), MW 2,115.

Kukamilika kwa miradi ya kuzalisha umeme ikiwemo mradi wa Rusumo na miradi mingine ya umeme iliyopo katika hatua za kukamilishwa, kutachangia ongezeko la kiwango cha umeme katika gridi ya Taifa. Hali itakayoimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii. Ongezeko la miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme limewezesha kaya nyingi kuunganishwa na umeme, hali inayochochea shughuli za uzalishaji na kuongeza kipato. Uzalishaji wa umeme kutoka MW 1,694.55 mwaka 2021/22 hadi kufikia MW 2,373 mwaka 2023/24 ikiwa lengo ni kufikia MW 4,915 mwaka 2025/26 kama ilivyobainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Mafanikio hayo yatachochea kuongezeka kwaa fedha za kigeni zitakazotokana na kuuza umeme kwa nchi jirani. Aidha, tayari Tanzania imekamilisha kuunganisha Gridi ya Taifa na gridi za nchi jirani za Kenya, Burundi na Rwanda na kazi ya kuunganisha na nchi ya Zambia inaendelea kupitia mradi wa TAZA. Hatua ambayo itawezesha kuuza ziada ya umeme katika nchi jirani. Mahitaji ya umeme ni MW 1766.96, hivyo kufanya kuwa na ziada ya MW 606.04.

Serikali kupitia REA imeunganisha umeme katika vijiji 12,167 kati ya 12,318 sawa na asilimia 94.5 na vitongoji 32,827 kati ya 64,359 sawa na asilimia 51. Upatikanaji wa umeme vijijini utachochea shughuli za kiuchumi na kijamii ikiwemo uanzishwaji wa miradi midogo midogo ya kipato kwa wananchi na kuharakisha kasi ya kupunguza umaskini. Hatua hizi zitaongeza uzalishaji viwandani, uchumi jumuishi na shindani, uwekezaji na biashara pamoja na kuimarika kwa maendeleo ya watu. Aidha, ili kuhakikisha utunzaji endelevu wa mazingira na uboreshaji wa afya za wananchi, Serikali inaendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi katika kupikia kwa kuzindua na kuanza kutekelezwa kwa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia ya Mwaka 2024 – 2034. Mkakati huo umewezesha zaidi ya mitungi 100,000 ya gesi ya kupikia (LPG) kugawiwa kwa wananchi katika mwaka 2023/24.

Uzalishaji wa umeme katika Mradi wa JNHPP (MW 2,115) umewezesha fungamanisho la sekta ya nishati na sekta ya uchukuzi kwa kuwa ni chanzo cha nishati ya kuendeshea treni ya kisasa ya SGR na hivyo kuongeza ufanisi katika usafiri na usafirishaji na hatimaye kuchangia katika matokeo makubwa ya kuongeza ushindani, uzalishaji viwandani na kuchochea biashara na uwekezaji.

**Jedwali 3.3: Viashiria na Shabaha za Utekelezaji katika Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Uzalishaji wa Umeme (MW) | 1,601.84 | 1,605.86 | 1,694.55 | 1,872.05 | 2,373 | 4,018 | 4,915 |
| 2. | Idadi ya Mikoa Iliyounganishwa na Gridi | 23 | 23 | 23 | 24 | 24 | 24 | 26 |
| 3. | Urefu wa Gridi ya Taifa (km) | 5,851.17 | 6,111.27 | 6,111.27 | 6,363.27 | 7,745.4 | 8,245.4 | 9,351 |
| 4. | Kupungua kwa Upotevu wa Umeme (%) | 16.19 | 15.16 | 14.71 | 14.62 | 14.56 | 14.5 | 7.9 |
| 5. | Asilimia ya Watu waliofikiwa na Umeme | 78.4[1] | - | - | - | - | - | 85 |
| 6. | Idadi ya Vituo vya CNG | 1 | 2 | 3 | 4 | 6 | 8 | 35 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Nishati*

### *3.2.2.5 Sekta ya Kilimo*

Sekta ya Kilimo ni moja ya sekta yenye uwezo wa kujumuisha sekta nyingi kwenye uchumi, pamoja na kuwa chanzo kikuu cha upatikanaji wa chakula nchini. Sekta hii ni moja ya chanzo cha kuzalisha malighafi kwa ajili ya viwanda, kutoa ajira kwa watu wengi, upatikanaji wa fedha za kigeni, na pia ni soko la bidhaa za viwandani.

Utekelezaji wa miradi katika sekta ya kilimo ulilenga kuongeza mchango kwenye Pato la Taifa, kuongeza ajira hususan kwa vijana na wanawake, kuongeza kipato kwa wakulima, na kuongeza mapato ya fedha za kigeni. Katika utekelezaji huo, ukuaji wa sekta ulifikia asilimia 4.2 ikilinganishwa na lengo la asilimia 6.1; mchango wa sekta kwenye pato la Taifa ulifikia asilimia 26.5 ikilinganishwa na lengo la asilimia 23.4; mchango wa mauzo nje ulifikia asilimia 16.1 ikilinganishwa na lengo la asilimia 19.0; na kiwango cha ajira kilifikia asilimia 65.6.

Matokeo haya yanaashiria kuwa juhudi zaidi zitahitajika kufikia malengo yaliyowekwa kwenye Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Hatua zinazoendelea kuchukuliwa ni pamoja na kutoa ruzuku za pembejeo, kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji na kupanua wigo wa masoko ya mazao na bidhaa ndani na nje ya nchi ili kuongeza kasi ya kufikia malengo yaliyowekwa na kuongeza ushindani katika masoko, uzalishaji viwandani na kuvutia uwekezaji na biashara.

1 Takwimu hizi ni kwa mujibu wa Taarifa ya Utafiti kuhusu Hali ya Upatikanaji na Matumizi ya Nishati Tanzania Bara (Energy Access and Use Situation Survey II Report, Tanzania Mainland) ya Mwaka 2019/20

**Jedwali 3.5: Viashira na Shabaha ya Utekelezaji wa Sekta ya Kilimo**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Kiwango cha Wastani wa Ukuaji (%) | 4.4 (2019) | 4.9 (2020) | 3.9 (2021) | 3.3 (2022) | 4.2 (2023) | 5.1 | 6.1 |
| 2. | Asilimia katika Pato la Taifa (bei za sasa) | 27.1 (2019) | 26.7 (2020) | 26.8 (2021) | 26.2 (2022) | 26.5 (2023) | 24.5 | 23.4 |
| 3. | Uwiano wa ajira za katika sekta ya kilimo kwa jumla ya Ajira katika sekta zote | 62.1 (2019) | 61.5 (2021) | 65.6 (2021) | 63.1 (2022) | 63.4 (2023) | 61 | 60 |
| **Mazao** | | | | | | | | |
| 1. | Wastani wa Ukuaji (%) | 4.7 | 4.2 | 3.1 | 3.5 | 3.7 | 4.7 | 5.7 |
| 2. | Asilimia katika Pato la Taifa (bei za sasa) | 14.9 (2019) | 15.1 (2020) | 15.1 (2021) | 15 (2022) | 16.1 (2023) | 13 | 12.3 |
| 3. | Hekta za Umwagiliwa | 694,715 | 695,005 | 695,005 | 727,280.6 | 727,280.6 | 983,465.46 | 1,200,000 |
| 4. | Mbegu zilizoidhinishwa na zilizozalishwa | 76,285.56 | 44,581.08 | 50,747 | 58,807.61 | 71,356 | 80,000 | 140,000 |
| 5. | Akiba ya taifa ya chakula (tani) | 52,724.730 | 107,384.057 | 141,575.902 | 46,893.983 | 340,478.908 | 1,150,000 | 700,000 |
| 6. | Kiasi cha mazao ya bustani yaliyozalishwa (tani) | 6,597,863 (2019) | 7,560,010 (2020) | 7,304,723 (2021) | 7,723,116 (2022) | 8,438,273.9 (2023) | 9,000,000 | 14,600,000 |
| 7. | Kiasi cha uzalishaji wa mazao ya biashara ya asili (traditional)(tani). | 1,144,631 (2019) | 1,058,798 (2020) | 898,967 (2021) | 973,436 (2022) | 1,267,160 (2023) | 1,610,000 | 1,583,200 |
| 8. | Idadi ya viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika | 113 | 183 | 195 | 252 | 328 | 333 | 338 |
| 9. | Idadi ya vyama vya ushirika vinavotumia mfumo wa soko rasmi | 1202 | 1302 | 1402 | 1573 | 2,231 | 2,626 | 2,782 |
| 10 | Idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika (milioni) | 4.2 | 4.5 | 5.1 | 6.2 | 6.9 | 8.3 | 14.5 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Kilimo*

### *3.2.2.6 Sekta ya Mifugo*

Sekta ya Mifugo ni moja ya sekta muhimu katika kujenga uchumi imara wa Taifa kwa kuongeza uhakika wa chakula cha kaya, kipato, afya bora ya mifugo na hivyo kuchangia uzalishaji wa malighafi kwa ajili ya sekta ya viwanda. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano umeweka vipaumbele vitakakavyoimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma. Hatua muhimu zinazotekelezwa zinahusisha kuongeza idadi na uwezo wa viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo kwa kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi pamoja na juhudi zitakazoongeza tija katika uzalishaji wa mifugo. Hii ni pamoja na ujenzi wa miundombinu muhimu ya malisho, majosho na masoko; huduma za ugani; udhibiti wa magonjwa na uzalishaji wa mbegu bora.

Utekelezaji wa vipaumbele hivyo unaopimwa na viashiria muhimu vikiwemo kuongezeka kwa mauzo ya mazao ya mfugo nje ya nchi, kiwango cha malighafi kinachochakatwa, kiwango cha chanjo ya mifugo, na mchango wa sekta ya mifugo katika Pato la Taifa vimeonesha mabadliko. Kiwango cha Wastani wa Ukuaji wa sekta umeendelea kuwa asilimia 5 katika mwaka 2023, na kuchangia asilimia 6.2 kwenye Pato la Taifa ikilinganishwa na malengo ya mpango ya asilimia 6.8 ifikapo mwaka 2025/2026; mauzo ya nyama nje yameongezeka kutokana na ongezeko la viwanda vya nyama vinavyouza nje kutoka vitatu (3) mwaka 2020 mpaka kufikia viwanda saba (7) mwaka 2024; kuongezeka kwa uzalishaji na usindikaji wa maziwa na hivyo unywaji wa maziwa na ulaji wa mazao yatokanayo na maziwa kuongezeka kutoka lita 54 kwa mtu kwa mwaka hadi kufikia lita 67.5 kwa mtu kwa mwaka (mwaka 2024).

Matokeo haya yametokana na ongezeko la uwekezaji katika sekta ya mifugo kutokana na kuimarika kwa mazingira bora ya uwekezaji katika sekta hii. Aidha, ongezeko la mazao ya mifugo yanayochakatwa na kuuzwa nje ni ishara kwamba malengo ya mpango ya kuimarisha viwanda yanafikiwa na bidhaa za Tanzania zinakuwa shindani katika masoko ya Kimataifa. Vilevile, ongezeko la ulaji na unywaji wa bidhaa za mifugo nchini ni ishara ya sekta ya mifugo kuchangia katika kuboresha lishe, hususan kiashiria cha kuongezeka ulaji wa mazao yatokanayo na mifugo kuongeza protini inayotokana na wanyama kama ilivyobainishwa kwenye Mpango Jumuishi wa Kitaifa wa Lishe Tanzania (National Multisectoral Nutrition Action Plan 2021/22 -2025/2026).

**Jedwali 3.6: Viashira na Shabaha ya Utekelezaji wa Sekta ya Mifugo**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Kiwango cha Wastani wa Ukuaji (%) | 4.9 | 5.0 | 5.0 | 5.0 | 5.0 | 5.5 | 6.5 |
| 2. | Mchango katika Pato la Taifa (bei za sasa) (%) | 7.4 | 7.1 | 7.2 | 6.7 | 6.2 | 6.2 | 7.0 |
| 3. | Kiwango cha Vifo vya Mifugo (%) | 27 | 24 | 21 | 18 | 16 | 16 | 12 |
| 4. | Kiwango cha Magonjwa ya Mifugo (%) | 6 | 5 | 4.5 | 3.5 | 2.5 | 2.5 | 3 |
| 5. | Kiwango cha Uogeshaji Mifugo katika josho (%) | 70 | 72 | 74 | 75 | 78 | 82 | 85 |
| 6. | Kiwango cha Chanjo ya Mifugo (%) | 25 | 37 | 39.5 | 40 | 42 | 42 | 50 |
| 7. | Wastani wa uzalishaji maziwa, Ng'ombe wa Asili (Lita) | 2 | 0.5 | 0.5 | 0.5 | 0.8 | 0.85 | 4 |
| 8. | Ngozi bora iliyochakatwa (%) | 10 | 15 | 20 | 25 | 30 | 40 | 50 |
| 9. | Uzalishaji wa Nyama (Tani) | 702,000 | 738,165.99 | 769,966.65 | 803,264.3 | 963,856.55 | 1,124,449 | 951,700 |
| 10. | Uzalishaji wa Maziwa katika (Lita bilioni) | 3.01 | 3.1 | 3.4 | 3.6 | 3.97 | 4.1 | 4.3 |
| 11. | Asilimia ya Maziwa yaliyochakatwa | 5 | 2 | 2 | 2 | 2.2 | 2.2 | 14 |
| 12. | Ngozi na ngozi Zilizochakatwa (Tani) | 1,190 | 143 | 146 | 2,250 | 2,385 | 2,900 | 9,210.6 |
| 13. | Mauzo ya nyama nje ya nchi (Tani) | 692 | 1,774.00 | 10,415.00 | 12,243.79 | 14,701.10 | 14,900 | 7,200 |
| 14 | Usafirishaji wa Ngozi (Tani) | 6,747 | 7,951 | 7,371 | 4,491 | 5,778 | 7,200 | 8,000 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Mifugo na Uvuvi*

### *3.2.2.7 Sekta ya Uvuvi*

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano umeweka dhamira ya kufanya mageuzi katika sekta ya uvuvi yakijuimuisha uwezo wa kutumia fursa ya uchumi wa rasilimali za maji, hususan bahari na maji baridi. Maeneo ya kipaumbele ya sekta yanajumuisha uvuvi katika maji baridi na bahari, kilimo cha majini, uhifadhi wa maeneo tengefu na uboreshaji wa uvuvi

baharini katika kina kirefu. Uvuvi ni miongoni mwa sekta zinazoimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji wa huduma kwa kuzalisha bidhaa zitakazotumia malighafi na rasilimali zinazopatikana nchini.

Baadhi ya hatua zitakazowezesha mageuzi hayo ni kuwezesha ununuzi wa meli na ujenzi wa bandari ya uvuvi; kuwezesha sekta binafsi kuanzisha na kukarabati viwanda vya mazao ya uvuvi; kuwezesha na kuhamasisha uwekezaji katika miundombinu ya uvuvi, vifaa na ufugaji wa kibiashara wa samaki; na kufungamanisha utafiti, ugani, uvuvi na kilimo cha majini.

Katika mwaka 2023, sekta ilichangia asilimia 1.7 katika Pato la Taifa na ilikua kwa asilimia 1.4 ikilinganishwa na lengo la kufika asilimia 1.9 na 8.4 mtawalia ifikapo mwaka 2025/26. Thamani ya mazao ya uvuvi yaliyouzwa nje ya nchi yamefika Dola za Marekani 298,945,553.12 mwaka 2023/24; ulaji wa samaki kwa kila mtu kufikia kilo 8.5 na kuchangia asilimia 30 ya ulaji wa kila siku wa protini ya wanyama ikilinganishwa na lengo la kilo 10.5 na asilimia 35 mtawalia ifikapo mwaka 2025/2026.

Uwekezaji katika sekta ya uvuvi umeleta matokeo chanya ikijumuisha kuongezeka kwa uzalishaji wa samaki, ajira, na mapato ya kiuchumi kwa wananchi na Pato la Taifa, ujenzi wa miundombinu kama viwanda vya kusindika samaki, na bandari. Aidha, sekta ya uvuvi huchangia usalama wa chakula, lishe bora, na ukuaji wa uchumi kupitia uzalishaji na usindikaji wa bidhaa za majini. Vilevile, uvuvi umechangia mapato ya utalii kupitia utalii wa ikolojia katika hifadhi za bahari na maeneo tengefu kupitia program za Royal Tour na kuchangia kuongezeka idadi ya watalii kutoka 38,160 mwaka 2022/23, hadi 40,088 mwaka 2023/24.

**1.7%**
**(2023)**
*sekta ya uvuvi ilichangia asilimia hiyo katika pato la taifa*

**$298mil**
**(2023/24)**
*thamani ya mazao ya uvuvi yaliyouzwa nje ya nchi*

**kilo 8.5**
**(2023/24)**
*wastani wa ulaji wa samaki kwa kila mtu*

**Jedwali Na. 3.7: Viashiria na Shabaha vya Utekelezaji wa Sekta ya Uvuvi**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Kiwango cha Wastani wa Ukuaji (%) | 6.3 | 6.7 | 2.6 | 1.9 | 1.4 | 4.5 | 8.4 |
| 2. | Asilimia katika Pato la Taifa (Bei za sasa) | 1.8 | 1.7 | 1.8 | 1.8 | 1.7 | 1.9 | 1.9 |
| 3. | Asilimia katika Mapato yatokanayo na Mauzo Nje | 3.0 | 3.4 | 3.2 | 3.3 | 3.4 | 3 | 4.5 |
| 4. | Ulaji kwa kila Mtu | 8.5 | 7.8 | 8.22 | 7.80 | 7.9 | 8.5 | 10.5 |
| 5. | Mchango katika Ulaji wa Protini ya Wanyama Kitaifa | 30 | 30 | 30 | 30 | 30 | 33 | 35 |
| 6. | Uzalishaji wa samaki (tani) | 497,567.28 | 493,850.24 | 502,305.34 | 513,218.90 | 530,379.66 | 575,000 | 600,000 |

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 7. | Idadi ya viwanda vya kusindika samaki | 12 | 15 | 17 | 20 | 21 | 21 | 17 |
| 8. | Idadi ya vituo vya kilimo majini (Aquaculture Development Centres - ADC) | 9 | 9 | 9 | 9 | 9 | 12 | 12 |
| 9. | Uzalishaji wa chakula cha samaki (tani) | 276.7 | 472.47 | 1,615.5 | 3,012.7 | 4,200 | 5,000 | 8,000 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Mifugo na Uvuvi*

### *3.2.2.8 Sekta ya Uzalishaji Bidhaa Viwandani*

Sekta ya Viwanda inategemewa kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii katika kuelekea kuwa nchi ya kipato cha kati. Viwanda ni sekta yenye uwezo wa kuzalisha ajira kutokana na ufungamanaji na sekta zingine kama vile kilimo, madini, mifugo katika hatua za uongezaji wa thamani. Uongezaji wa thamani wa mazao ghafi na kuzalisha bidhaa za viwandani ni mhimili imara wa biashara.

Utekelezaji wa miradi katika sekta ya viwanda na biashara ulilenga kuongeza mchango wa sekta katika Pato la Taifa; ukuaji wa sekta; kuongeza ajira; na mapato ya mauzo ya nje.

Utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unaonesha kuwa mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa ulifikia asilimia 7 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la asilimia 8.5 ifikapo 2025/26; ukuaji wa sekta ya viwanda ulifikia asilimia 4.3 ikilinganishwa na lengo la asilimia 6.8 mwaka 2025/26; na mchango katika mapato ya mauzo nje ulifikia asilimia 17.7 ikilinganishwa na lengo la asilimia 19 mwaka 2025/26. Mwenendo huu wa utekelezaji utaongeza ushindani, uzalishaji viwandani na kuvutia uwekezaji na biashara.

**7.0%**
**(2023/24)**
*mchango wa sekta ya viwanda katika pato la taifa*

**8.5%**
**(2025/26)**
*mchango wa sekta ya viwanda katika pato la taifa kwa miaka ijayo*

**Jedwali 3.8: Viashira na Shabaha ya Utekelezaji wa Sekta ya Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Mchango katika Pato la Taifa (%) | 8.2 | 8.4 | 7.8 | 7.1 | 7.0 | 8.5 | 8.5 |
| 2. | Kiwango cha ukuaji halisi wa Pato la Taifa (%) | 5.2 | 4.7 | 4.5 | 4.2 | 4.3 | 6.8 | 6.8 |
| 3. | Mchango katika Ajira Zote (%) | 7.4 (2019) | 8.5 (2020) | 8.0 (2021) | 8.0 (2022) | 8.1 (2023) | 12.8 | 12.8 |
| 4. | Mchango katika Mapato ya Mauzo Nje (%) | 17.1 | 17.7 | 22.9 | 26.9 | 17.7 | 19 | 19 |
| 5. | Mchango wa bidhaa zilizozalishwa viwandani kwa teknolojia ya kati katika mauzo nje (%) | 28 | 29.2 | 21.1 | | 25 | 42 | 39 |
| 6. | Mchango wa bidhaa zilizozalishwa viwandani kwa teknolojia ya juu katika mauzo nje (%) | 8 | 8.8 | 8.9 | | 25 | 39 | 10 |
| 7. | Mchango katika Mauzo yote nje (%) | 16.9 (2019) | 17.7 | 22.9 | 26.9 | 21.6 | 24 | 24 |
| 8. | Kiasi cha ukuaji halisi cha pato la Taifa (%) | 1,180 | 908.6 | 1213.2 | 1419.2 | 1363.3 | | 2114 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Viwanda na Biashara*

### *3.2.2.9 Sekta ya Madini*

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kufanyika kwa mageuzi makubwa katika sekta ya madini ikiwemo kuimarisha usimamizi na udhibiti wa uchimbaji; kuwezesha wachimbaji wadogo; kuimarisha taasisi za utafiti; kuongeza ushiriki katika biashara ya madini; kuhamasisha uongezaji thamani; na kuwezesha uchimbaji wa madini muhimu na ya kimkakati duniani.

Utekelezaji wa afua katika sekta ya madini unaonesha kuwa ukuaji wa sekta ya madini ulifikia asilimia 11.3 mwaka 2023 sawa na asilimia 93.9 ya lengo la asilimia 11.6 ifikapo mwaka 2025/26; mchango kwenye pato la Taifa ulifikia asilimia 9.0 mwaka 2023 sawa na asilimia 51.1 ya lengo la asilimia 11.2 ifikapo mwaka 2025/26; mchango katika mapato ya fedha za kigeni zitokanazo na mauzo ya bidhaa nje ya nchi ulifikia asilimia 56.2 mwaka 2023 ikiwa imevuka lengo la asilimia 51.7 ifikapo mwaka 2025/26.

Mwenendo huu wa utekelezaji wa afua katika sekta ya madini unaashiria ufanisi wa mageuzi yaliyofanyika, hali inayojitokeza kwenye ongezeko la uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje; uwazi kwenye biashara kupitia masoko na vituo vya ununuzi wa  ya madini; na kuongezeka kwa ajira.

**Jedwali 3.9: Viashira na Shabaha ya Utekelezaji wa Sekta ya Madini**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Wastani wa Ukuaji (%) | 5.2 | 6.7 | 9.6 | 10.9 | 11.3 | 11.0 | 11.6 |
| 2. | Mchango kwenye Pato la Taifa (%) | 17.7 | 6.7 | 7.2 | 9.1 | 9.0 | 10.7 | 11.2 |
| 3. | Jumla ya Mapato ya Fedha za Nje (Dola za Marekani milioni) | 2,280.5 | 3,310.7 | 3,046.2 | 3,395.3 | 3,551.4 | 3,654.4 | 3,760.4 |
| 4. | Mauzo ghafi nje (%) | 15 | | | | 9 | 7 | 5 |
| 5. | Bidhaa zilizoongezwa thamani (%) | 85 | | | | | 93 | 95 |
| 6. | Mchango katika mapato yote ya fedha za nje yatokanayo na mauzo ya bidhaa  nje (%) | 45.2 | | 45.9 | 56.0 | 56.2 | 50.2 | 51.7 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Madini*

### *3.2.2.10 Sekta ya Mazingira na Maliasili Asilia*

Mazingira na maliasili asilia ni msingi wa maendeleo endelevu. Serikali kupitia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuimarisha mifumo ya utunzaji wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali asilia kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Utekelezaji wa afua hizi umechangia katika Pato la Taifa kutokana na matumizi endelevu ya misitu, maji na rasilimali za bahari kwa asilimia 4.1 mwaka 2023/24 ikilinganishwa lengo la asilimia 7 mwaka 2025/26. Vile vile, zimechangia kukabiliana na athari za mazingira na mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuboresha afya za wananchi kutokana na matumizi ya nishati safi. Aidha zimeongeza uwezo wa kufanya biashara ya kaboni hivyo kuongeza mapato kwa jamii na Serikali.

**Jedwali 3.10: Viashiaria na Shabaha ya utekelezaji wa sekta ya Usimamizi wa Mazingira na Maliasili Asilia**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Wastani wa Ukuaji (%) | 4 | 2.7 | 2.6 | 2.7 | 2.5 | 6 | 7 |
| 2. | Mchango katika Pato la Taifa kutokana na matumizi endelevu ya misitu, maji na rasilimali za bahari | 4 | 3.2 | 3.5 | 3.1 | 4.1 | 6 | 7 |
| 3. | Kiwango cha kupungua kwa uharibifu wa misitu (Reduced Deforestation Rate) (Ha.) | 469,420 | 469,420 | 469,420 | 469,420 | 469,420 | 469,420 | 234,710 |
| 4. | Maeneo ya misitu ya kibishara (commercial forest Plantation) yaliyoanzishwa (Ha) | 500,000 | 507,274 | 507,274 | 507,274 | 507,274 | 510,000 | 550,000 |
| 5. | Asilimia ya miradi mikubwa inayokidhi uchambuzi wa athari kwa mazingira (EIA) na kanuni za ukaguzi | 90 | 100 | 100 | 100 | 100 | 93 | 65 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Makamu wa Raisi*

### *3.2.2.11 Sekta ya Utalii*

Sekta ya Utalii inayojumuisha hifadhi na mbuga za wanayamapori, maeneo tengefu, ukanda wa Bahari kumbi za mikutano, ni moja ya sekta muhimu inayotoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulilenga kuendeleza mazao mapya ya utalii kwa ajili ya ukuaji wa uchumi endelevu; na kuendeleza kanda ya utalii ya kusini mwa Tanzania.

Utekelezaji wa afua hizi umewezesha kuongeka kwa mchango wa sekta ya utalii kufikia 17.2 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la asilimia 17.9 mwaka 2025/26; kuongezeka idadi ya watali kufikia 3,784,214 (Watalii wa

ndani ya nchi ni 1,976,009 na Watalii kutoka nje ya nchi ni 1,808,205) mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la watalii 5,000,000 mwaka 2025/26 na kuongezeka kwa kiwango cha mchango wa fedha za kigeni kufikia asilimia 25 ikilinganishwa na lengo la asilimia 27 mwaka 2025/26.

Hatua zilizochukuliwa zimeleta matokeo katika kuongeza kipato cha mtu moja moja kutokana na ajira milioni 3.6 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja. Vile vile sekta hii imetoa mchango wa ukuaji wa sekta nyingine hususan usafiri na biashara ndogo ndogo pamoja na ongezeko la uwekezaji hususan hoteli ma migahawa.

**Jedwali Na. 3.11: Viashiria na Shabaha za Utekelezaji vya Sekta ya Utalii**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Mchango katika Pato la Taifa (bei za sasa) (%) | 17.5 | 14.9 | 10.1 | 13.0 | 17.2 | 17.5 | 18.9 |
| 2. | Idadi ya Watalii kutoka nje ya nchi | 1,527,230 | 620,867 | 922,692 | 1,454,920 | 1,808,205 | 2,062,431 | 5,000,000 |
| 3. | Idadi ya Watalii ndani ya nchi | 959,831 | 788,933 | 2,363,260 | 1,084,737 | 1,976,009 | | |
| 4. | Wastani wa idadi ya siku za kulala mtalii. | 13 | 10 | 10 | 9 | 10 | 10 | 14 |
| 5. | Wastani wa Matumizi ya Mtalii kwa Siku (USD) | 216 | 115 | 141 | 166 | 276 | 260 | 326/455 |
| 6. | Mchango katika Mapato ya Fedha za Kigeni (%) | 25 | 5.3 | 21 | 25 | 25 | 26 | 27 |
| 7. | Mapato yatokanayo na Watalii (Dola za Marekani bilioni) | 2.6 | 0.7 | 1.3 | 2.5 | 3.4 | 4.1 | 6.0 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Maliasili na Utalii*

### *3.2.2.12 Sekta ya Sanaa, Michezo na Ubunifu*

Sekta ya Sanaa, Michezo na Ubunifu inahusisha kundi la vijana wengi ambalo ndio sehemu kubwa ya idadi ya watanzania. Sekta hii ina nguvu kubwa ya ushawishi, uhamasishaji na ustawishaji wa jamii na maendeleo ya nchi na kuwa na mvuto mkubwa kwa makundi mbalimbali ya jamii hususan vijana wanaounda sehemu kubwa ya nguvu kazi ya nchi. Shughuli za sekta hii ni muhimu pia katika kutoa fursa za ajira na kipato kwa vijana.

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuweka mazingira rafiki ili kuchochea ukuaji, kuzalisha ajira na kuongeza mchango wa sekta katika Pato la Taifa. Kutokana na utekelezaji wa afua, sekta ilikua kwa asilimia 17.7 na mchango wa asilimia 0.4 katika ukuaji wa Pato la Taifa; kuongezeka miundombinu ya michezo kufikia 63 ikilinganishwa na lengo la miundombinu 72 mwaka 2025/26; na kuongezeka miundombinu ya mazoezi kufikia 35 ikilinganishwa na lengo la miundombinu 40 mwaka 2025/26. Hatua hizi zinatarajiwa kuwa na wasanii na wana michezo wengi, wenye ubora na wabunifu na hatimaye kuwa na jamii yenye vipaji vingi na vya juu, inayoelimika, yenye ufahamu na yenye uwezo wa kushindana kimataifa.

**Jedwali 3.12: Viashiaria na Shabaha vya Utekelezaji wa Sanaa, Utamaduni na Michezo**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya miundombinu ya michezo na iliyoboreshwa nchini kote | 63 | 1 | 1 | 3 | 7 | 20 | 72 |
| 2. | Majengo mawili changamani ya Sanaa na Michezo Makao Makuu ya Nchi, Dodoma na Dar es Salaam. | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| 3. | Idadi ya miundombinu iliyojengwa/kukarabatiwa katika Chuo cha Kuendeleza Michezo Malya na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamaoyo (TaSUBa). | 35 | 13 | 15 | 17 | 13 | 6 | 40 |
| 4. | Idadi ya filamu na muziki zilizoidhinishwa, kusambazwa na kutumika | 15,303 | 2,962 | 3,763 | 3,201 | 4,070 | 1,672 | 25,735 |
| 5. | Idadi ya wasanii waliosajiliwa katika tasnia ya ubunifu | 3,462 | 469 | 368 | 955 | 1,219 | 1,500 | 8,666 |

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 6. | Eneo Changamani la Sanaa, Kiromo, Bagamoyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| 7. | Idadi ya wataalamu katika tasnia ya ubunifu waliopata mafunzo | 2,852 | 450 | 442 | 500 | 10,837 | 11,500 | 4297 |
| 8. | Idadi ya michezo na mashindano ya kimataifa yaliyoandaliwa na Tanzania kushiriki | 178 | 0 | 98 | 135 | 157 | 110 | 350 |
| 9. | Idadi ya vibali vilivyotolewa kwa vyama vya michezo na wanamichezo binafsi | 178 | 0 | 57 | 45 | 194 | 110 | 400 |
| 10. | Jumba Changamani la Filamu. | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| 11. | Idadi ya wanariadha wanaocheza nje ya nchi | 54 | - | 21 | 31 | 17 | 30 | 150 |
| 12. | Idadi ya wageni wanaoendesha shughuli za kuzalisha filamu nchini Tanzania. | 359 | 60 | 87 | 100 | 64 | 70 | 1,059 |
| 13. | Idadi ya wasanii/ wataalamu katika tasnia ya ubunifu/makundi yanayofanya maonesho yao nje ya nchi | 1,620 | 330 | 430 | 461 | 467 | 300 | 1755 |
| 14. | Idadi ya wasanii wa nje/ wataalamu katika tasnia ya ubunifu wanaofanya maonesho yao nchini Tanzania | 720 | 142 | 153 | 162 | 167 | 100 | 2,312 |
| 15. | Idadi ya wataalamu wa Kiswahili wanaofanya kazi nje ya Tanzania | 56 | 64 | 71 | 95 | 111 | 150 | 656 |
| 16. | Idadi ya machapisho ya Kiswahili yaliyouzwa nje ya nchi | 200 | 252 | 2189 | 1640 | 242 | 250 | 700 |
| 17. | Idadi ya tuzo za kimataifa zilizoandaliwa na kutolewa kwenye utamaduni, sanaa na tasnia ya ubunifu | 47 | 38 | 41 | 188 | 62 | 113 | 130 |

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 18. | Idadi ya vikundi vya utamaduni na sanaa kutoka nje ya nchi vilivyoshiriki katika matamasha ya Kimataifa yanayoandaliwa kila mwaka na TaSUBa. | 5 | 4 | 4 | 6 | 23 | 110 | 20 |
| 19. | Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika Chuo cha Kuendeleza Michezo Malya | 300 | 439 | 533 | 684 | 758 | 800 | 1,300 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo*

### *3.2.2.13 Sekta ya Kukuza Uwekezaji na Biashara*

Katika kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, moja ya kipaumbele kilichobainishwa ni kukuza uwekezaji na biashara. Kipaumbele hiki kinahusu kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara.

Uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji umepewa kipaumbele katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kama msingi imara katika kuchochea uchumi shindani na shirikishi na kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, ili kukuza uwekezaji na biashara. Mpango umebainisha hatua kadhaa zitakazoimarisha uwekezaji, miongoni mwa hizo ni kurahisisha michakato ya uwekezaji na biashara; kupunguza gharama za uwekezaji na biashara; na kuboresha mifumo ya ukusanyaji na usambazaji wa taarifa za biashara na masoko; kupunguza gharama za biashara kwa kuimarisha ufanisi wa miundombinu ya usafirishaji, mamlaka za udhibiti na watoa huduma; na kuboresha uwezeshaji wa biashara na kupunguza vihatarishi vya biashara kwa kutumia mifumo ya kidigitali katika mnyororo wa thamani.

Baadhi ya viashiria muhimu vinavyopimwa katika eneo la uwekezaji na biashara ni idadi ya miradi inayosajiliwa na thamani yake; ajira zinazozalishwa; na kiasi cha ardhi ya uwekezaji iliyotengwa. Vingine ni mchango mauzo ya nje katika Pato la Taifa; mchango wa bidhaa za viwandani katika mauzo nje; na mchango wa huduma katika mauzo nje. Aidha, miradi 9,678 ya uwekezaji yenye thamani ya dola za Marekani milioni 8,658 imesajiliwa katika kipindi cha mwaka 2023 ikilinganishwa na miradi 8,401 yenye thamani ya dola za Marekani milioni 5,658.47 kwa mwaka 2022. Miradi hii imesajiliwa kupitia TIC, Tume ya Madini, EPZA, TANESCO, BRELA, BOT, TMDA, na EWURA. Sheria sita (6) za Sekta ya Sanaa zimefanyiwa tathmini kwa lengo la kupima kama malengo ya kutungwa kwa sheria hizo yamefikiwa

katika kuhakikisha kuwa Sekta ya Sanaa inakua ya kibiashara na yenye tija kwa wasanii na Taifa.

Kama ilivyoainishwa kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, ushiriki wa Sekta Binafsi katika utoaji huduma za kijamii na uchumi ni kiungo katika ustawi wa jamii na ukuaji wa uchumi endelevu. Vilevile, ukuaji wa uwekezaji na biashara unasaidia kukuza uvumbuzi na teknolojia mpya zinazochochea ushindani katika shughuli za uzalishaji na biashara. Uwekezaji na biashara huhamasisha maboresho na ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano na usafirishaji ambayo inawezesha usafirishaji wa bidhaa, huduma na watu kwa kuunganisha maeneo magumu kufikika hivyo kuongeza ufanisi wa huduma kwa jamii kama vile benki, bima, na elimu, na hatimaye kuimarisha uchumi na kuboresha maisha ya watu.

Uwekezaji umesaidia kutoa ajira 442,249 zinazotokana na uwekezaji katika sekta mbalimbali sawa na asilimia 176.9 ya lengo la mwaka 2026. Vile vile, uwekezaji katika shughuli za kilimo umewezesha upatikanaji wa malighafi katika shughuli za viwanda kwa asilimia 65. Hivyo, shughuli hizo zinachangia katika ukuaji wa sekta, maendeleo ya watu na uchumi kwa ujumla.

**Jedwali 3.13: Viashira na Shabaha ya Utekelezaji wa Sekta ya kukuza uwekezaji na biashara**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya Miradi ya Uwekezaji iliyosajiliwa na TIC na EPZA | 230 | 249 | 305 | 378 | 737 | 640 | 600 |
| 2. | Thamani ya Miradi ya Uwekezaji (Dola za Marekani) | 2,680.71 | 3,449.03 | 2,371.68 | 5,450.64 | 6,796.09 | 8,813 | 8,500 |
| 3. | Idadi ya Ajira kutokana na Miradi ya Uwekezaji | 49,055 | 39,123 | 50,282 | 55,741 | 248,048 | 280,000 | 250,000 |
| 4. | Idadi ya Kongano za Uwekezaji | 10 | 12 | 13 | 14 | 27 | 21 | 5 |
| 5. | Idadi ya Miongozo ya Uwekezaji ya Mikoa | 13 | 7 | | 2 | | 26 | 26 |
| 6. | Idadi ya Ofisi za Utoaji Huduma Mahala Pamoja | 11 | 13 | 13 | 13 | 13 | 15 | 18 |
| 7. | Kiasi cha Ardhi ya Uwekezaji iliyotengwa (ekari) | 90,990 | 98,861 | 99,735 | 159,813 | 214,972.94 | 391,030.94 | 528,917 |
| 8. | Idadi ya Makongamano ya Uwekezaji Kimataifa | 21 | 49 | 63 | 89 | 204 | 180 | 150 |

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 9. | Idadi ya Maboresho ya sheria na kanuni za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji yaliyofanywa | | 35 | 42 | 55 | 66 | 80 | 88 |
| 10. | Idadi ya maboresho ya kufuta au kupunguza tozo, ada na ushuru katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji yaliyofanywa | | 218 | 232 | 307 | 374 | 383 | 388 |

***Chanzo:*** *Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji*

### *3.2.2.14 Sekta ya Diplomasia ya Uchumi*

Tanzania imechukua hatua muhimu za kuimarisha mahusiano na nchi nyingine kulingana na vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Hatua hizo zinajumuisha kuimarisha diplomasia ya uchumi, siasa, mtengamano wa Kikanda na Kimataifa na kupanua wigo na taswira ya Tanzania kimataifa. Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua mbalimbali ni pamoja na: Kuendelea kupatikana kwa misaada na mikopo yenye masharti nafuu kutoka taasisi na mashirika ya kimataifa, kuongezeka kwa watalii wanaokuja Tanzania; kubidhaishwa kwa lugha ya kiswahili na hivyo kuongeza upatikanaji wa ajira za wakalimani na walimu wa Kiswahili.

**Jedwali 3.14 Viashira na Shabaha ya Utekelezaji wa Sekta ya Diplomasia ya Uchumi**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya mikutano kati ya Tanzania na nchi moja moja, ya kikanda na kimataifa iliyoshiriki | 30 | 32 | 80 | 90 | 101 | 110 | 250 |
| 2. | Idadi ya watanzania walioshiriki katika ulinzi wa amani nje ya nchi | - | - | 1401 | 1401 | 1532 | 1500 | 3,500 |
| 3. | Idadi ya ofisi na nyumba za kuishi zilizokarabatiwa | - | 4 | 4 | 4 | 4 | 4 | 14 |

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 4. | Idadi ya Hati za Makubaliano ya Pamoja zilizosainiwa kati ya Tanzania na nchi nyingine | 12 | 32 | 33 | 66 | 78 | 84 | 80 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki*

### *3.2.2.15 Sekta ya Elimu na Maendeleo ya Ujuzi*

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unalenga katika kuendeleza rasilimali watu, kuchochea uchumi shindani na shirikishi. Ili kufikia malengo hayo, mpango umejielekeza katika kuboresha mifumo ya elimu na kuwianisha elimu na mahitaji ya soko la ajira, ikijumuisha kuchochea uvumbuzi na uhawilishaji wa teknolojia.

Pamoja na mambo mengine, mpango ulibainisha hatua mahususi ambazo zitatekelezwa kila mwaka zikijumuisha kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote; kuhuisha na kuandaa mitaala kuendana na soko la ajira; kuwezesha matumizi ya TEHAMA katika kufundisha na kujifunza katika ngazi zote za elimu; na kuboresha miundombinu ya elimu na vifaa katika ngazi zote.

Kutokana na utekelezaji wa afua hizo, kuna ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa elimu ya msingi, wanaojiunga na kidato cha kwanza, kupungua kwa mdondoko wa wanafunzi katika ngazi mbalimbali za elimu kutokana na Serikali kuboresha miundombinu na kuongeza idadi ya walimu. Vilevile , ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi na wanufaika wa mikopo katika ngazi mbalimbali za elimu ya juu na wanafunzi wa astashahada kutaongeza nguvu kazi mahiri katika Uchumi. Aidha, matokeo ya mabadiliko ya kisera yaliyofanyika katika mwaka 2023 yanayolenga kuboresha elimu ili iendane na mahitaji halisi ya soko la ajira yataanza kuonekana zaidi katika kipindi cha muda wa kati kutokana na utekelezaji wake kufanyika kwa hatua. Mabadiliko haya yatawezesha Tanzania kuzalisha rasilimali watu mahiri katika nyanja mbalimbali kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi.

**Jedwali 3.15: Viashiria na Shabaha ya Utekelezaji wa Sekta ya Elimu**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Kiwango cha uandikishaji jumla (% ya wanaostahili) –Awali | 78.5 | 76.9 | 83.87 | 89.46 | 89.62 | 90 | 91 |
| 2. | Idadi ya walimu wenye sifa – Msingi | 178,122 | 180,706 | 172,156 | 174,398 | 190,515 | 283,873 | 284,000 |
| 3. | Idadi ya walimu wenye sifa – Sekondari | 84,614 | 87,992 | 84,700 | 95,800 | 98,919 | 98,919 | 100,000 |
| 4. | Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa mwalimu – Msingi | 1:62 | 1:63 | 1:63 | 1:62 | 1:56 | 1:61 | 1:60 |
| 5. | Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa kitabu – Msingi | 1:4 | 1:3 | 1:2 | 1:2 | 1:2 | 1:2 | 1:1 |
| 6. | Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa darasa - Msingi | 1:81 | 1:81 | 1:77 | 1:75 | 1:63 | 1:70 | 1:60 |
| 7. | Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa darasa – Sekondari | 1:46 | 1:47 | 1:39 | 1:37 | 1:35 | 1:37 | 1:37 |
| 8. | Idadi ya wanafunzi waliopata mikopo ya elimu ya juu | 132,392 | 145,000 | 177,892 | 202,016 | 220,278 | 233,000 | 180,000 |
| 9. | Idadi ya wahitimu wa vyuo vikuu | 60,940 | 51,228 | 48621 | 54810 | 57742 | 56520 | 70,001 |
| 10. | Kiwango cha udahili jumla - Vyuo vya Ufundi (%) | 4.5 | 4.6 | 4.8 | 4.9 | 5.2 | | 6 |
| 11. | Idadi ya wanafunzi wanaohitimu kwa mwaka - Vyuo vya Ufundi | 55,501 | 103,896 | 123,919 | 125,498 | 128,654 | | 120,000 |
| 12. | Asilimia ya wanafunzi wanaohitimu masomo ya sayansi na uhandisi kwa mwaka | 36 | 38.7 | 41.4 | 44.9 | 45.6 | | 40 |

***Chanzo:*** *Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*

### *3.2.2.16 Sekta ya Afya*

Sekta ya Afya ni muhimu katika kukuza uchumi na maendeleo ya watu. Sekta hii inahusisha maendeleo ya rasilimali watu na uwezo wao wa kushiriki katika kukuza uchumi na ustawi wa jamii. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka mitano ulilenga kupanua upatikanaji na ubora wa huduma za afya vijijini na mijini kwa kujenga na kukarabati miundombinu ya huduma za afya na upatikanaji wa wataalamu wa afya.

Utekelezaji wa afua za sekta ya afya umewezesha kupunguza idadi ya vifo vitokanavyo na uzazi kufikia 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022 na kuvuka lengo la vifo 180 mwaka 2025/26; kuongezeka kwa wastani wa idadi ya uzazi uliohudumiwa na mfanyakazi wa afya mwenye ujuzi kufikia 84 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la asilimia 85 kwa kila vizazi 1000 mwaka 2025/26. Mafanikio hayo yamechangiwa na kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma ya afya; kuboreshwa kwa miundombinu; ununuzi wa vifaa na vifaa tiba; kusogeza huduma za afya karibu zaidi na jamii na kuongeza ajira katika sekta ya afya.

Aidha, wastani wa umri wa kuishi umeongezeka kutoka miaka 67.6 (2023) hadi makadirio ya miaka 68.3 (2024) ambayo ni ushahidi wa kutosha wa utekelezaji wa afua mbalimbali katika sekta ya afya.

**Jedwali 3.16: Viashiria na Shabaha ya Utekelezaji kuhusu Sekta ya Afya**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya vifo vya watoto wachanga kwa kila vizazi hai 1000 | 26 (2010 TDHS) | 25 (2015-16 TDHS-MIS) | 24 (2015-16 TDHS-MIS) | 24 (2022 TDHS-MIS) | 24 (2022 TDHS-MIS) | 15 | 15 |
| 2. | Idadi ya vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa kila vizazi hai 1000 | 81 (2010 TDHS) | 67 (2015-16 TDHS-MIS) | 43 (2022 TDHS-MIS) | 43 (2022 TDHS-MIS) | 43 (2022 TDHS-MIS) | 43 | 40 |
| 3. | Uzazi uliohudumiwa na mfanyakazi wa afya mwenye ujuzi | 80 | 92.3 | 93.6 | 94.4 | 94.6 | 85 | 85 |
| 4. | Wastani wa umri wa kuishi (miaka) | 66.1 | 66.7 | 65.4 | 67.6 | 68.3 | 68.3 | 68 |
| 5. | Kiwango cha maambukizi ya VVU kitaifa (%) | 4.7 | 4.9 | 4.9 | 4.9 | 4.4 | 4.4 | 3.1 |
| 6. | Matumizi ya Serikali katika huduma za afya (%) | 10 | | 9.1 | 7 | 8 | 9 | 12.2 |

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 7. | Idadi ya vifo vitokanavyo na uzazi kwa kila vizazi hai 100,000 | 454 (2010 TDHS) | 530 (2015-16 TDHS-MIS) | 220 | 220 | 104 (2022 TDHS-MIS) | 100 | 180 |
| 8. | Matumizi ya Serikali katika afya (% ya matumizi yote ya Serikali) | 10 | 10.6 | 7.29 | 7.9 | 8 | 9 | 12.2 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Afya na Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

### *3.2.2.17 Sekta ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira*

Huduma ya maji na usafi wa mazingira ni miongoni mwa mahitaji muhimu yanayochochea maendeleo ya watu. Sekta hii inahusisha upatikanaji na usambazaji wa maji pamoja na utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano umetoa kipaumbele katika upatikanaji na usambazaji wa maji safi na salama vijijini na mijini pamoja na utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji.

Matokeo ya utekelezaji wa afua katika sekta ya maji na usafi wa mazingira yanaonesha kuwa asilimia ya idadi ya watu wa vijijini wanaopata maji ya bomba au maji yaliyolindwa kama chanzo kikuu kimefikia asilimia 79.6 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la asilimia 85 mwaka 2025/26; uwiano wa kaya za vijijini zenye miundombinu iliyoboreshwa ya usafi wa mazingira imefikia asilimia 77.5 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la asilimia 60.0 mwaka 2025/26; asilimia ya watu katika jiji la Dar es Salaam wanaopata huduma ya maji ya bomba au maji salama kama chanzo chao kikuu kimefikia asilimia 92.5 ikilinganishwa na lengo la asilimia 95.0 mwaka 2025/26; Asilimia ya watu katika makao makuu ya mikoa wanaopata maji ya bomba au maji yaliyolindwa imefikia asilimia 90.0 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la asilimia 95.0 mwaka 2025/26; na asilimia ya kaya katika makao makuu ya mikoa iliyounganishwa kwenye mfumo rasmi wa maji-taka imefikia asilimia 14.0 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la asilimia 30.0 mwaka 2025/26.

Matokeo haya yatachangia kufikiwa kwa malengo yalianishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**79.6%**
**(2023/24)**
*asilimia ya watu wa vijijini wanaopata maji ya bomba*

**77.5%**
**(2023/24)**
*asilimia ya kaya vijijini zenye miundombinu bora ya mazingira*

**92.5%**
**(2025/26)**
*asilimia ya watu dar es alaam wanapata maji salama*

**14.0%**
**(2023/24)**
*asilimia ya kaya katika mikoa iliyounganishwa na mfumo wa maji taka*

**Jedwali Na.3.17:Viashiria na Shabaha vya Utekelezaji wa sekta ya Usambazaji wa Maji na Huduma za Usafi wa Mazingira**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Asilimia ya idadi ya watu wa vijijini wanaopata maji ya bomba au maji yalivyolindwa kama chanzo kikuu | 70 | 72.3 | 74.5 | 77 | 79.6 | 83 | 85 |
| 2. | Uwiano wa kaya za vijijini zenye miundombinu iliyoboreshwa ya usafi wa mazingira | 36 | 47.3 | 60.4 | 73.5 | 77.5 | 82 | 60 |
| 3. | Asilimia ya watu katika makao makuu ya mikoa wanaopata maji ya bomba au maji yaliyolindwa | 84 | 85 | 86.5 | 88 | 90 | 92.5 | 95 |
| 4. | Asilimia ya kaya katika makao makuu ya mikoa iliyounganishwa kwenye mfumo rasmi wa maji-taka | 13 | 11 | 13 | 13 | 14 | 15 | 30 |
| 5. | Asilimia ya upotevu wa maji (NRW) katika makao makuu ya mikoa | 30 | 36.8 | 35.7 | 35.3 | 35.3 | 30 | 20 |
| 6. | Asilimia ya watu katika makao makuu ya wilaya na miji midogo wanaopata huduma ya maji ya bomba au maji yaliyolindwa kama chanzo kikuu | 70 | 67 | 72 | 73.4 | 74.5 | 80 | 85 |
| 7. | Asilimia ya watu katika jiji la Dar es Salaam wanaopata huduma ya maji ya bomba au maji salama kama chanzo chao kikuu | 85 | 87 | 89 | 90 | 92.5 | 93 | 95 |
| 8. | Asilimia ya kaya katika jiji la Dar es Salaam waliounganishwa kwenye mfumo rasmi wa maji-taka | 13 | 13 | 11 | 13 | 12.4 | 16 | 30 |

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 9. | Kiwango cha upotevu wa maji (NRW) katika jiji la Dar es Salaam | 35 | 38.3 | 39.2 | 41.5 | 39.5 | 35 | 20 |
| 10. | Idadi ya vyanzo vya maji vilivyotengwa na kutangazwa kwa ajili ya ulinzi na uhifadhi | 18 | 18 | 34 | 34 | 59 | 80 | 200 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Maji*

### *3.2.2.18 Sekta ya Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuendeleza upimaji wa maeneo ya makazi, biashara, uwekezaji na huduma za jamii. Hii ni kwa kutambua kuwa ardhi iliyopimwa na kupangwa ni kichocheo cha shughuli za kiuchumi na kijamii, maendeleo ya makazi na miji, uhifadhi wa mazingira na udhibiti wa mabadiliko ya tabianchi, na hivyo kuchangia kufikiwa kwa matokeo katika maeneo ya vipaumbele vya kitaifa.

Utekelezaji wa afua katika mipango miji, nyumba na maendeleo ya makazi umeleta matokeo yafuatayo: Asilimia ya ardhi iliyopimwa imefikia 26 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la asilimia 37.0 mwaka 2025/26; Idadi ya leseni za makazi zilizotolewa katika makazi yasiyo rasmi ilifikia 27,895 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la idadi ya leseni 20,000 mwaka 2025/26; Uwiano wa vijiji vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi umefikia asilimia 52.7 mwaka 2023/24 na hivyo kufikia lengo lililowekwa ifikapo mwaka 2025/26; na Idadi ya ramani za msingi zilizohuishwa kwa eneo imefikia 30 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la idadi ya ramani za msingi 26 mwaka 2025/26.

Utekelezaji huu utawezesha kukamilika kwa mipango ya matumizi ya ardhi na hivyo kuchangia kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja, kuongeza uwekezaji na kupunguza migogoro katika jamii.

**26%**
**(2023/24)**
*asilimia ya ardhi iliyopimwa nchini*

**27,895**
**(2023/24)**
*idadi ya leseni za makazi zilizotolewa*

**52.7%**
**(2025/26)**
*asilimia ya uwiano wa vijiji vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi*

**Jedwali 3.18: Viashiria na Shabaha vya utekelezaji wa sekta ya Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya mali zilizorasimishwa katika makazi yasiyo rasmi | 1,551,716 | 1,754,822 | 2,207,627 | 2,469,686 | 2,623,888 | 2,634,375 | 3,134,375 |
| 2. | Asilimia ya eneo la ardhi yenye makazi yasiiyo rasmi | 70 | 70 | 70 | 67.3 | 67.3 | 67.3 | 50 |
| 3. | Eneo la ardhi lilitengwa na kulindwa kwa matumizi ya umma (ekari) | 858,665 | 858,665 | 858,665 | 756,110.74 | 756,110.74 | 756,110.74 | 1,000,000 |
| 4. | Idadi ya miji yenye mipango kabambe ya upimaji iliyohishwa | 24 | 25 | 27 | 28 | 28 | 29 | 47 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*

### *3.2.2.19 Sekta ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii*

Sekta ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii inajumuisha matokea ya afua za hifadhi ya jamii; chakula na lishe; uongozi na utawala wa sheria; mifumo ya utoaji haki; amani, utulivu, na usalama; kuendeleza ujuzi na shughuli za bunge. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuwawezesha na kuwashirikisha wananchi kiuchumi, na kuboresha mazingira ya watu wenye mahitaji maalumu ili kupunguza umaskini wa kipato na utegemezi. Aidha mpango unahimiza jamii kuwekeza katika uzalishaji wa chakula na lishe bora ili kupunguza matatizo ya kiafya. Mpango unatambua kuwa Uongozi Bora ni msingi wa maendeleo ya Taifa. Aidha mpango unatambua kuwa mifumo ya utoaji na upatikanaji wa haki ni muhimu katika kuimarisha usawa na ustawi wa jamii na kwamba maendeleo na ustawi wa Taifa yanategemea amani, utulivu na usalama; na kutambua mchango wa mhimili wa bunge katika kufikia matokeo tarajiwa ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Utekelezaji wa afua katika sekta hizi umekuwa na matokeo yafuatayo: Idadi ya vituo vya malezi ya watoto vilivyosajiliwa vimefikia 4,068 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la vituo 7,500 mwaka 2025/26; Kiwango cha kupungua kwa uhalifu nchini kimefikia asilimia 4.3 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la asilimia 35 mwaka 2025/26; na Idadi ya watu waliosajiliwa na kutambuliwa na NIDA imefikia milioni 24.9 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la milioni 34.1 mwaka 2025/26.

Mafanikio haya yamechangia kukinga jamii kutumbukia katika umaskini uliokithiri; kuwa na uhakika wa chakula na lishe bora; kuongeza na kuimarisha uwajibikaji; ulinzi na upatikanaji wa haki; na mazingira bora ya biashara na uwekezaji.

**Jedwali 3.19: Viashiria na Shabaha vya utekelezaji wa sekta ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya vituo vya malezi ya watoto vilivyosajiliwa | 1,543 | 1,543 | 2,714 | 3,233 | 4,068 | 4,800 | 7,500 |
| 2. | Idadi ya wazee wasiojiweza wanaopata huduma za bima ya afya bure | 166,866 | 166,866 | 201,509 | 262,513 | 365,284 | 432,642 | 574,321 |
| 3. | Idadi ya watoto wanaolelewa baada ya mapatano | 12,068 | 12,068 | 26,903 | 32,905 | 46,473 | 48,051 | 50,000 |
| 4. | Kiwango cha kupungua kwa uhalifu nchini (%) | 5.2 | - 7.5 | - 1.9 | 4.3 | 3.2 | 35 | |
| 5. | Idadi ya watu waliosajiliwa na kutambuliwa na NIDA | 22,194,288 | 23,185,729 | 23,965,371 | 24,897,459 | 27,286,749 | 34,080,610 | |

***Chanzo:*** *Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalum*

### *3.2.2.20 Kuendeleza Ujuzi*

Ujuzi ni nyenzo muhimu katika kufikia maendeleo ya uchumi kwa kutoa fursa za ajira, kukuza uzalishaji na ubunifu, kuvutia uwekezaji na kupunguza umaskini. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kukuza ujuzi na uwezeshaji ili kukabiliana na kiwango kidogo cha ujuzi miongoni mwa nguvu kazi na kuwezesha kujiajiri au kuajirika na kuwa na kiwango cha ujuzi wa kumudu ushindani katika soko.

Katika kipindi cha utekelezaji wa mpango, afua zilizotekelezwa ni pamoja na Mafunzo ya Kukuza Ujuzi kwa Njia ya Uanagenzi (ApprenticeshipTraining); Mafunzo ya Uzoefu wa Kazi kwa Wahitimu (Internship Training); Mafunzo ya Kuongeza Ujuzi kwa Wafanyakazi (Upskilling); Urasimishaji wa ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo (Recognition of Prior Learning Skills); na Kukuza kazi za Staha nchini. Matokeo ya afua hizi umechangia kupatikana kwa ajira 3,221,352 kupitia Taasisi za umma na Binafsi na kuunganishwa kwa watu 3,463 na fursa

za ajira nje ya nchi kwa kushirikiana na Mawakala Binafsi wa Ajira. Vijana 41,886 walipatiwa mafunzo ya uwezeshaji ujuzi na stadi za kazi. Matokeo mengine ni utoaji wa ruzuku kwa vyama vya watu wenye ulemavu 13; na mikopo yenye thamani ya shilingi 3,197,403,492 kwa Vikundi/ Makampuni 148 ya vijana.

Utekelezaji wa afua zinazohusiana na ukuzaji ujuzi na uwezeshaji umezalisha nguvu kazi yenye ujuzi kwa ajili ya kufanya kazi katika maeneo ya kazi na uzalishaji viwandani na kuchangia katika kujenga uchumi imara na thabiti wenye uwezo wa kuhimili ushindani na kujenga uwezo wa vijana kujiajiri na kuajiriwa na kupata kipato cha kuwawezesha kujikimu. Hii imechangia katika dhamira ya kufikia maisha bora kwa wote kama ilivyoainishwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

**Jedwali 3.18: Viashiria na Shabaha vya utekelezaji wa sekta ya Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya watu wenye mafunzo ya uanagenzi | 46,200 | 14,440 | 22,200 | 11,973 | 6,300 | 231,000 | 46,200 |
| 2. | Idadi ya watu wanaotumia teknolojia ya kisasa kwenye kilimo | 40,000 | 8,980 | 4,480 | - | - | 200,000 | 40,000 |
| 3. | Idadi ya Watu walioshiriki mafunzo ya Utarajali (Internship) | 30,000 | 4,136 | 5,742 | 3,864 | 474 | 150,000 | 30,000 |

***Chanzo:** Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu)*



> Huduma ya maji na usafi wa mazingira ni miongoni mwa mahitaji muhimu yanayochochea maendeleo ya watu.





# VIPAUMBELE NA MALENGO KWA MWAKA 2025/26

## 4.1 Utangulizi

Maandalizi ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 yanaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inayolenga kuwezesha Tanzania kuingia katika kundi la nchi za uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 na kuwa na kiwango cha juu cha maendeleo ya watu. Mpango huu ni wa tano na wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Hivyo, mapendekezo ya mpango yamejikita katika kuendeleza na kukamilisha utekelezaji wa afua zinazotoa matokeo ya maeneo matano ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Vilevile, Mpango huu ni kiungo kati ya mipango inayokamilika na mipango mipya inayotarajiwa kutekelezwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Hivyo, mpango huu utazingatia kuainisha na kutekeleza afua muhimu ambazo hazikukamilika ili kuandaa mazingira shirikishi na endelevu kwa mipango ijayo kwa kufanya uchambuzi wa kina wa wadau (Asasi za Kiraia na Sekta Binafsi) watakaoshiriki katika kutekeleza mipango husika.

### Vigezo vya Kuchagua Vipaumbele vya Mapendekezo ya Mpango

Nguzo muhimu ya maandalizi ya Mapendekezo ya Mpango ni ukuaji wa uchumi pamoja na maeneo matano ya vipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Maandalizi ya vipaumbele vya Mpango yamezingatia vigezo vifuatavyo:

i. Ukuaji Endelevu wa Uchumi: Hii inalenga kufikia ukuaji wa uchumi wa juu wenye ustahimilivu zaidi kwa kuongeza tija, mahitaji ya jumla na kupanua shughuli za kiuchumi nchini kote kwa kulenga uwekezaji wa kimkakati katika sekta muhimu (kilimo, viwanda na huduma).

ii. Kupunguza Umaskini: Hii inalenga kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi jumuishi unaozingatia upatikanaji wa huduma za kijamii, programu zinazolenga kinga ya jamii na zenye kutengeneza fursa za kiuchumi na ulinzi wa haki milki za mali na ubunifu (property rights).

iii. Kuzalisha Ajira kwa Wananchi: Hii inahusisha kuainisha afua zitakazoimarisha ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi zilizopo na zinazoanzishwa ili kutengeneza nafasi za ajira zitakazotokana na uwekezaji mpya na ubunifu ili kutumia nguvu kazi inayokua hususan vijana na wanawake.

iv. Kuimarishwa kwa Ushindani katika Masoko ya Kikanda na Kimataifa: Hii inajumuisha kuboresha miundombinu, kuweka mazingira wezeshi ya biashara, kufuata taratibu za kimataifa, kuimarisha rasilimali watu, kukuza uwekezaji wa ndani na nje na kutumia teknolojia zinazoibukia kupitia maendeleo ya miundombinu ya TEHAMA ili kuchochea ukuaji wa uchumi wa kidijitali.

v. Maendeleo Endelevu: Kuhakikisha matumizi endelevu ya maliasili na kupunguza uharibifu wa mazingira na upotevu wa viumbe hai.

vi. Utawala Bora na Utawala wa Sheria: Hii inajumuisha hatua madhubuti za kupunguza rushwa, kuwezesha upatikanaji wa haki, kuimarisha uwajibikaji, kulinda haki za binadamu, kuheshimu uhuru wa kujieleza, kukuza usawa na haki, kuimarisha demokrasia na kuhakikisha utekelezaji wa taratibu na mifumo jumuishi. Aidha, Mifumo ya majadiliano (Public Private Dialogue) itaimarishwa ili kutoa fursa za kuboresha utoaji wa huduma kwa uwazi.

Vipaumbele vinayopendekezwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026 vimezingatia malengo tarajiwa na matokeo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

## 4.2 Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi

Uchumi shindani unahusisha kujenga jamii yenye uwezo wa kushindana kitaifa, kikanda na kimataifa; kuimarisha utulivu na uendelevu wa viashiria vya uchumi jumla; kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara; kuchochea uvumbuzi na uhawilishaji wa teknolojia za ndani na za kimataifa; kuimarisha haki milki za ubunifu na mali; na kuendeleza miundombinu na huduma za reli, barabara, madaraja, usafiri wa majini, usafiri wa anga, TEHAMA, nishati, bandari na viwanja vya ndege. Aidha, matumizi ya TEHAMA katika nyanja zote za kijamii na kiuchumi yataimarishwa. Hivyo, afua zilizolengwa kuchochea uchumi shindani katika maeneo haya zitaendelea kutekelezwa. Vipaumbele hivyo ni pamoja na:

i. Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Reli ikiwemo reli ya SGR pamoja na uimarishaji wa huduma za usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo;
ii. Ujenzi wa miundombinu ya barabara kuu na za mikoa; barabara za kimkakati na za kupunguza foleni;
iii. Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya TEHAMA na kuboresha huduma kwa kushirikiana na watoa huduma na wadau wengine wa Sekta Binafsi;
iv. Ununuzi wa ndege, ujenzi na ukarabati wa meli za abiria na mizigo katika maziwa makuu na bahari pamoja na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege na bandari ili kuimarisha huduma za usafiri na usafirishaji katika maziwa, bahari, mito na anga;
v. Uzalishaji, wa nishati ya umeme kutoka vyanzo mbalimbali na teknolojia ya matumizi ya nishati safi;
vi. Kuimarisha miundombinu ya usafirishaji umeme ikiwemo kuunganisha mikoa ambayo haipo katika Gridi ya Taifa;
vii. Usambazaji wa umeme kwa vijijini vilivyobakia;
viii. Utafutaji gesi asilia na ujenzi wa miundombinu ya uchakataji;
ix. Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi;
x. Kuimarisha utoaji wa huduma za hali ya hewa; na
xi. Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa Fedha za Kigeni na kulinda thamani ya shilingi dhidi ya dola za Marekani.

## 4.3 Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma

Eneo hili linajumuisha uongezaji thamani ya mazao mbalimbali pamoja na kuzalisha bidhaa zitakazotumia malighafi na rasilimali zinazopatikana nchini pamoja na afua zinazolenga kuboresha huduma za utalii, fedha na bima. Vipaumbele vinavyopendekezwa ni:

i. Utafutaji na uhamasishaji wa uwekezaji wa madini ya kimkakati yakiwemo madini ya chuma na magadi soda;
ii. Ujenzi na ukarabati wa maeneo Maalumu ya Uwekezaji na Kanda Maalum za Kiuchumi;
iii. Ukuzaji tija,uchakataji,uimarishaji masoko katika kilimo, mifugo na uvuvi na utafutaji wa masoko kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini;
iv. Kukuza tafiti katika sekta zenye uwezo mkubwa wa kuzalisha malighafi za viwanda;
v. Kuimarisha uwezo wa uhifadhi wa chakula;
vi. Upatikanaji wa taarifa za jiosayansi kupitia tafiti zinazohusu uwepo wa madini nchini;
vii. Kutambua, kukuza na kuwezesha uchimbaji wa madini adimu na ya kimkakati;
viii. Kujenga uwezo wa nchi kuhimili na kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi;
ix. Ujenzi wa miundombinu ya utalii ikiwemo barabara, mawasiliano, huduma za afya, na usalama wa watalii;

x. Kutekeleza mikakati ya kulinda viwanda vya ndani ili kuvutia wawekezaji; na
xi. Kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma kwa kuboresha mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu kwenye maeneo ya viwanda (industrial clusters) kwa ajili ya viwanda vidogo na vya kati.

## 4.4 Kukuza Uwekezaji na Biashara

Katika mwaka 2025/26, Serikali itaendelea kutekeleza shughuli ambazo hazikukamilika katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kama ifuatavyo:

i. Kuimarisha mifumo kwa ajili ya kuchochea uwekezaji wa umma kwa kutunga Sera, Sheria, Kanuni, Mikakati na Miongozo;
ii. Kuimarisha upatikanaji wa huduma kwa wawekezaji katika ngazi zote;
iii. Kuboresha mazingira ya biashara ili kuvutia wawekezaji kutoka Sekta Binafsi;
iv. Kuimarisha mifumo ya kisheria na utoaji haki ili kujenga mazingira rafiki ya kisheria katika kuwezesha biashara na uwekezaji;
v. Kuimarisha uwekezaji wa kimkakati na kufungamanisha sekta zenye mnasaba na Uchumi wa Buluu;
vi. Kuimarisha usimamizi wa kanuni za kitalaam na viwango vya kimataifa;
vii. Kuboresha mifumo ya ukusanyaji na usambazaji wa taarifa za biashara na masoko;na
viii. Kuimarisha diplomasia ya uchumi.

## 4.5 Kuchochea Maendeleo ya Watu

Maendeleo ya watu ni matokeo ya utekelezaji wa afua katika sekta za elimu, afya maji na usafi wa mazingira; ustawi na maendeleo ya jamii; upangaji na upimaji wa ardhi; amani, utulivu na usalama.

Serikali katika mwaka 2025/26 itaendelea kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu, huduma za afya, maji na usafi wa mazingira nchini. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya ustawi na maendeleo ya jamii; ardhi na kudumisha amani, utulivu na usalama. Hivyo, Mpango utajielekeza katika maeneo yafuatayo:

i. Kuimarisha mifumo na usimamizi wa uendeshaji wa elimu ikiwemo mageuzi ya elimu, afya, maji na mazingira;
ii. Kuandaa rasilimali watu na kujenga miundombinu ya elimu, afya, maji na mazingira;
iii. Kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi;
iv. Kuimarisha na kuhamasisha uwekezaji katika programu za mtindo wa maisha na lishe bora;
v. Kujenga na kukarabati miundombinu ya michezo, sanaa na ubunifu.
vi. Kuongeza na kuboresha mazingira ya watu wenye mahitaji maalum pamoja na wigo wa hifadhi na kinga ya jamii;

vii. Kuongeza kasi ya upangaji, upimaji, umilikishaji na usajili wa ardhi mijini, vijijini na maeneo ya kimkakati;

viii. Kuendelea kutekeleza mapendekezo ya haki jinai ikiwemo kuboresha miundombinu ya utoaji haki nchini;

ix. Kuimarisha mifumo ya kubadili aina ya maisha kwa kuendelea kutekeleza programu za kuboresha maendeleo ya watu ikiwemo kutekeleza mkakati wa amsha ari;

x. Kuboresha mazingira ya utoaji huduma za kiutendaji, kiutawala na kisheria; na

xi. Kuimarisha usalama wa raia na mali zao ili kudumisha amani na utulivu nchini.

## 4.6 Kuendeleza Ujuzi

Katika mwaka 2025/26, Serikali itajikita katika kuwezesha ujuzi wa nguvu kazi kwa kuendelea na utekelezaji wa afua zinazohusiana na kukuza ujuzi na kuchochea ukuzaji wa fursa za ajira kwa vijana na watu wenye ulemavu. Utekelezaji wa afua hizo utazalisha nguvu kazi yenye ujuzi kwa ajili ya kufanya kazi katika maeneo ya uzalishaji viwandani na hivyo kuchangia katika kujenga uchumi imara wenye uwezo wa kuhimili ushindani. Vipaumbele kwa mwaka 2025/26 ni:

i. Kuwezesha na kuendeleza ujuzi kwa makundi mbalimbali katika ngazi zote za Elimu;

ii. Kuimarisha ujuzi katika majadiliano ya mikataba hususan ya mafuta, gesi na madini, uandishi wa Sheria, utafiti wa sheria na uendeshaji wa mashauri ya madai dhidi ya Serikali ndani na nje ya nchi na

iii. Kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Ujuzi wa Mwaka 2016/17 – 2025/26.

# SURA YA TANO





# UFUATILIAJI, TATHMINI NA VIHATARISHI

## 5.1 Utangulizi

Serikali imejipanga kuimarisha mfumo wa usimamizi wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo. Mfumo huu umejengwa katika nguzo tatu ambazo ni: kuainisha vipaumbele bayana na kwa uwazi kwa kila sekta; nidhamu ya utekelezaji; na uwajibikaji. Katika kuhakikisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 unakamilisha matamanio yaliyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 pamoja na malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali itaendelea kuratibu na kusimamia ufuatiliaji na tathmini ya miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa nchini. Lengo la ufuatiliaji na tathmini ni kuhakikisha uwazi kupitia takwimu sahihi zitakazoakisi thamani halisi ya fedha za programu na miradi pamoja na kupendekeza mbinu na mikakati ya kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa mradi. Vilevile, sura hii inajumuisha vihatarishi vya utekelezaji wa mpango na hatua za kukabiliana navyo.

Ufuatiliaji na Tathmini wa programu na miradi itahusisha hatua mbalimbali zikiwemo ukusanyaji wa taarifa, uchambuzi na utoaji wa taarifa kupitia mifumo mbalimbali ya ufuatiliaji na tathmini ikiwemo Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (NPMIS) pamoja na ufuatiliaji kwenye eneo la miradi. Vilevile, ufuatiliaji na tathmini utajumuisha miradi inayotekelezwa na Serikali pamoja na Sekta Binafsi kwa lengo la kuongeza na

kuimarisha ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika shughuli za kiuchumi pamoja na maendeleo ya nchi na kushirikisha watekelezaji wote wa programu na miradi hususan Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

## 5.2 Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 utazingatia miongozo ifuatayo: Sheria ya Bajeti, Sura 439; tathmini ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano; Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo wa Mwaka 2022; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26; Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma Toleo la Mwaka 2022 (PIM-OM); Mwongozo wa Usimamizi wa Tathmini Nchini wa Juni, 2024; Waraka Na. 5 wa Hazina wa Mwaka 2020/21 kuhusu Matumizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo; Waraka Na. 1 wa Hazina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti 2025/26 na Mpango Kazi na Mtiririko wa Mahitaji ya Fedha.

### 5.2.1 Matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na tathmini ni muhimu kwa mafanikio ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/26. Matokeo tarajiwa ya ufuatiliaji na tathmini ni: kuongeza uwajibikaji kwa kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali; kusaidia katika kufanya maamuzi sahihi kupitia taarifa za ufuatiliaji na tathmini; kutambua hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa programu na miradi; kurahisisha mgawanyo wa rasilimali; na kupima utendaji dhidi ya malengo yaliyowekwa.

### 5.2.2 Muundo wa Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini

Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuzingatia Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini. Mwongozo huo umeainisha mawanda na malengo ya mradi, hali ya utekelezaji, taarifa za ugharamiaji, taarifa za mikataba, changamoto na mapendekezo ya kukabiliana na changamoto hizo. Aidha, Tume ya Mipango itaendesha majadiliano na wadau yatakayosaidia katika uchambuzi wa matokeo ya ufuatiliaji na tathmini kwenye maeneo ya vipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26.

### 5.2.3 Mgawanyo wa Majukumu katika Ufuatiliaji na Tathimini

Ufuatiliaji na Tathmini ni suala mtambuka linaloshirikisha wadau mbalimbali katika utekelezaji kwa kuzingatia mgawanyo wa majukumu ulioanishwa kwenye Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo. Ufuatiliaji utafanyika kwa kutumia uchambuzi wa kina juu ya matokeo tarajiwa kupitia tafiti na takwimu zilizozalishwa na wadau mbalimbali ikiwemo Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Aidha, Tume ya Mipango itaendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya Kielelezo kwa kushirikiana na kuhusisha wadau muhimu na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya matokeo ya utekelezaji wa miradi na program katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu.

## 5.3 Vihatarishi na Mikakati ya Kukabiliana Navyo kwa Mwaka 2025/2026

Katika kuhakikisha kuwa malengo ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 yanatekelezwa kwa ufanisi na kuleta matokeo chanya, Serikali itajipanga kutekeleza mikakati ya kudhibiti vihatarishi vinavyoweza kujitokeza kwa kuzingatia Mwongozo wa Kuandaa Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi katika Sekta ya Umma (2023). Vihatarishi hivyo vimegawanyika katika makundi mawili (2) makuu ambayo ni: (i) vihatarishi vya ndani ambavyo vinaweza kusababishwa na utendaji au mifumo ya Serikali; na (ii) vihatarishi vya nje ya udhibiti wa Serikali.

### 5.3.1 Vihatarishi vya Ndani na Nje

Vihatarishi vya Ndani: Kukosekana kwa mifumo madhubuti ya ufuatiliaji na tathmini ya programu na miradi ya maendeleo; ushiriki usioridhisha wa sekta binafsi katika kutekeleza mipango ya maendeleo; kupanga na kutekeleza vipaumbele visivyoendana na Mipango ya Kitaifa; umiliki na migogoro ya ardhi; upotevu wa mapato ya Serikali unaotokana na biashara mtandao; mabadiliko ya viwango vya riba katika soko la fedha la ndani; na vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa rasilimali. Serikali ina uwezo wa kudhibiti kutokea au kukabili athari za vihatarishi hivi kupitia utekelezaji wa mikakati iliyowekwa.

Vihatarishi vya Nje: Mabadiliko ya tabianchi, majanga ya asili na magonjwa ya mlipuko; mitikisiko na mdororo wa kiuchumi duniani; kuongezeka kwa kiwango cha riba katika masoko ya kimataifa; migogoro na hali ya siasa inayojitokeza kwa nchi jirani, kikanda na kimataifa; kuongozeka kwa kasi ya mabadiliko ya teknolojia; na kupungua kwa mwenendo wa mikopo yenye masharti nafuu na misaada.

### 5.3.2 Mikakati ya Kukabiliana na Vihatarishi

Mikakati ya kukabiliana na vihatarishi vilivyobainishwa ni pamoja na: kuhakikisha miongozo ya ufuatiliaji na tathmini inazingatiwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kuhakikisha mipango ya kisekta inaendana na vipaumbele vya kitaifa; kuendelea kuboresha mazingira wezeshi ya biashara ili kuvutia uwekezaji; kuongeza matumizi ya kidigitali katika ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mifumo ya Serikali; kuchukua mikopo ya muda mrefu yenye masharti nafuu ili kuepuka athari ya kupanda kwa viwango vya riba; kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021; kuimarisha mikakati ya kisera ili kukabiliana na mabadiliko ya kiuchumi duniani ikijumiisha kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula, kama zao la ngano; na kuendelea kuboresha mifumo ya kisheria, kisera na kitaasisi ili iendane na ukuaji wa teknolojia.

Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango
Jengo la Kambarage Ghorofa ya 9,
1 Mtaa wa Kambarage
S. L. P. 1324
41104 Tambukareli, Dodoma

www.planning.go.tz

Tume ya Mipango Tanzania @planning_tz @planning_tz @planningtz